Tafsiri hiyo ya Katekisimo ndogo katika luga ya kiswahili imetengenezwa hapa Lubumbashi – R.DC, kutokeya Bureau de Coordination de Traduction ELCC henye kongozwa na wachungaji wafwatao :

1. Mchg YUMBA LUMBALA
2. Mchg Stéphane KAZADI WATENE
3. Mchg Albert MWAMBA KAMULETE
4. Mchg ILUNGA KABULO
5. Ndugu David KASONGO

## UTANGULIZI

Ona KATEKISIMO NDOGO YA Martin LUTHER na maelezo mbali mbali. Iliyoandikwa mwaka wa 1529, baada ya kutembelea ma kanisa ya jimbo lake.

Matembezi hayo iliweza kumuonesha kutoelewa kwa wa Kristo na wa chungaji wengi walio jifunza nao pamoja Theologia katika kanisa la kikatholique.

Luther akaona mara ngapi illfaa kuwa na muongozi ya kitabu kyenye maelezo wazi na hahisi kwa ukweli kubwa kwa imani ya kikristo.Dipo kitabu ndogo ya Katekisimo ina onekana mandiko yake, hahisi kwa vipande viwili ao tatu, na ili yenye kutangaziwa chini ya uongozi ya ma kanisa la kinjili la kilutheri-synod ya inchi ya Fransa na Belgique.

Inandikwa kutoka mistari ya kwanza kwenyi ukurasa 27 ya kitabu hiki. Tena inakuwa na mafasiriyo halali yenye kufaniwa kwa maulizo na ma jibu yambatanayo na wingi ya mandiko ya Biblia.

Mwanzo ya hii mafasiriyo ipatikanayo tena katika mandiko yenye kutangaza katika inchi ya KIFRANSA na ikabadilishwa kwa wakati ule kupitiya kwa Rev. W. De Moss, kwa wakati ya mutume ndani ya inchi Togo.

Tunashukuru wanzisho wa kazi nzuri.
Tuli ya chunguza na kubadilishwa kwa wakati wetu na nia mbili ifwatayo :
Ya kwaza, kwandika mandiko halali na nyepesi yenye kuwa na mafasiriyo tena na maneno yenye kweleweka na watu wote.
Ya pili, kuchunguza ma swali ya kipeke ya maana katika inchi ya ki Africa na kujibu ku ma swali tunayo jiuliza wakati tunapoishi katika maneno makubwa ya imani kwa vitu vyote.

Hii inaonesha maswali kama mwabudiyokwa Mungu pekee, dunia na hali ya kiroho na matumizi ya maombi, maana ya majaribu, na ndowa na kuwa na kwa wa bibi wawili. Kisha tuliongeza mwisho ya kitabu hiki horoza ya vitabu ya Biblia na lexique yenye kutafsiri maneno ya maana zaidi.
Hii ni msingi, na msingi rahisi, mwepesi na nguvu, ju yake kanisa la kilutheri inaweza kujenga kupitiya mafundisho ya kweli na ya furaha.

Basi twataka kitabu hiki kiwe na maendeleo mazuri, na tunaomba Mungu afanye kwa kitabu hiki ku watu wengi chemchem tajiri ya baraka.

W. Kreiss

Citation extraites de la Bible traduite par LOUIS SECOND Révision NEG – 1779, Copyrigh
©
Société Biblique de Genève, CP, CH –1211 Genève

EGLISE LUTHERIENNE DE CONFESSION
REPRESENTATION LEGALE

Tafsiri ya Katekisimo Ngodo ya Martin Luther katika lugha ya Kiswahili toka ki-fransa na ruhusa ya Lutheran Chuch-Missouri Synod
World Mission
1333 South Kirkwood Rood
Saint Louis,Mo 631122-7295 USA

Kupitia kwa pastor David KOENING.
PAR LE BUREAU DE COORDINATION DE TRADUCTION/E.L.C.C.
E-mail : elecotra@ yahoo.fr
LUBUMBASHI, Août 2004.

# I
# AMRI KUMI

**Jinsi bwana wa jamaa atafundisha kwa njia ya unyenyekevu kwa wale walio wake.**

**AMRI YA KWANZA**
MUNGU
"Usiwe na miungu mingine ila mimi"

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumwongopa, kumpenda na kumtegemea Mungu kuliko vitu vyote.

**AMRI YA PILI**
JINA LA MUNGU
"Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako"

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumwogopa na kumpenda Mungu, na hivyo tusilitukane jina lake. Kutukana jina la Mungu kwa kuapa, kwa kukufuru na kufanya uganga ao kuishi kwa uwongo na unafiki lakini kila wakati tuliite tuliombe, tulitukuze na kulishukuru kwa heshima.

**AMRI YA TATU**
NENO LA MUNGU
"Uikumbuke siku ya sabato uitakase"

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumwogopa na kumpenda Mungu kwa hiyo tusilizarahu Neno lake na mahubiri yake, lakini tulitakase na kwa furaha tulisikie na kujifunza Neno lake.

## AMRI YA INE

WAZAZI NA WA KUBWA

"Wa heshimu baba yako na mama yako siku zako zipate kuwa nyingi."

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumuongopa na kumpenda Mungu kwa hiyo, tusiwazarahu wazazi na wa kubwa wetu, wala tusiwakasirishe, ila tuwaheshimu, tuwatumikie, tuwapende na ku watii.

## AMRI YA TANO

UZIMA NA MAISHA YA JIRANI

"Usiue"

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumwogopa na ku mpenda Mungu na kwa hiyo tusi hatarishe maisha ya jirani yetu wala tusi mwumize, ila tumsaidie wakati eko katika hatari ao katika maitaji.

## AMRI YA SITA

UTAKASO NA NDOA

"Usizini"

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumwongopa na kumpenda Mungu. Kwa hiyo, imetupasa kuwa na maisha matakatifu na safi katika mafikili, Neno na tendo kila mmoja akimpenda na kumheshimu mke wake au mume wake katika ndoa.

**AMRI YA SABA**
MALI YA JIRANI
"Usiibe"

**Jibu** : Imetupasa kumwongopa na kumupenda Mungu na kwa hiyo, tusimwibie fedha au mali ya jirani yetu, wala tusimupunje au kufanya kwa njia yoyote ambayo haistahili, ila tumsaidie kuyaongeza na kuyalinda mapato na mali yake.

**AMRI YA NANE**
UKWELI NA UKUMU
"Usimshudie jirani yako kwa uongo"

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumwongopa na kumpenda Mungu kwa hiyo tusiseme uwongo juu ya jirani wala kumusaliti, kumsingizia au kumpotezea heshima, ila badala yake. Na tutazame mwenendo wake kwa upendo. Tuombe msamaha , tumsemee mema, na tumsaidie sifa yake isiharibike.

**AMRI YA TISA**
TAMAA NA MAWAZO MBAYA
"Usiitamani nyumba ya jirani yako"

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumwongopa na kumpenda Mungu. Kwa hiyo, tusifanye hila au kujipatia uriti au nyumba ya jirani yetu, wala kuipata kwa kuitumia vibaya sheria, bali tumhudumie, na kumsaidia ili apate kutunza vilivyo vyake vizuri.

**AMRI YA KUMI**
TAMAA NA MAFIKILI MBAYA

"Usi tamani mke wa jirani yako wala mtumishi wake wa kiume au mtumishi wake wa kike au ngombe wake au punda wake au chochote kilicho cha jirani yako"

Ina maana gani ?

**Jibu** : Imetupasa kumwogopa na kumpenda Mungu. Hivyo, tusimnyaganye, tusimchukize au kushawishi mke, watumishi au ngombe wa jirani yetu, lakini tuwasaidie waendelee kumtumikia.

**MWISHO YA AMRI KUMI**
MUNGU ANASEMA NINI KUHUSU AMRI HIZI ZOTE ?

**Jibu** : Mungu anasema : "Mimi Bwana Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu ; na wapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha ine cha wanichukizao; lakini na waonyesha upendo thabiti kwa maelfu wanipendao, na kuzishika amri zangu." (Kutoka 20 : 5 – 6)

Maana yake nini ?

**Jibu** : Mungu anaogofya na kuwaadhibu wote wanaoziasi amri zake. Hivyo tuogope ghadhabu yake, na tusiziasi amri zake. Kwa upande mwingine ana waahidia neema na kila baraka wote wanao zitunza. Kwa hiyo, tumpende, tumtegemee, na tufanye kwa furaha aliyoyaagiza.

✞ ✞ ✞

# II

# UKIRI

**Jinsi Bwana wa jamaa atakavyofundisha waliyo wake kwa unyenyekevu.**

## FUNGU LA KWANZA
## UUMBJI.

"Namwamini Mungu Baba Mwenye enzi Muumba mbingu na dunia"

Hii ina maana gani ?

**Jibu :** Naamini ya kwamba Mungu ndiye aliyeniumba mimi na vyote vilivyomo, kwamba amenipa na anahifadhi mwili na roho yangu, viungo vyote na akili, mawazo yangu na welekevu wangu wote wa akili, tena hunipa mavazi na chakula, nyumba, jamaa na vitu vyote ipashwayo maisha yangu yote siku kwa siku. Ananikinga kwa hatari zote kunilinda na kuniokowa katika uovu wo wote. Na hayo yote ananifanyia kwa sababu ya wema na rehema yake ya kimungu iliyo kama ya baba. Sikuyastahili mimi kwa hivyo vyote, imenipasa kumshukuru na kumsifu, kumtumikia na kumtii. Hii ni kweli kabisa.

## FUNGU LA PILI
## UKOMBOZI

"Na katika Yesu Kristo, Mwana wa pekee, Bwana wetu aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu akazaliwa na Bikira Mariamu, akateswa wakati wa Pontio Pilato, alisulubiwa, akafa na kuzikwa, alishuka kuzimu siku ya tatu alifufuka toka kwa wafu, akapaa mbinguni ameketi mukono wa kuume wa Mungu Baba Mwenye enzi kutoka huko atakuja kuwaukumu waliyo hai na wafu."

Hii ina maana gani ?

**Jibu :** Nina amini kwamba Yesu Kristo ni Mungu kweli. Mwana wapekee wa Baba tangu milele na pia mwanadamu kweli aliye zaliwa naye Bikira

Mariamu, huyu ndiye Bwana wangu aliyeniokoa nilipo potea na kustahili kuhukumiwa. Amenikomboa na kunitoa katika dhambi zote na mauti na nguvu ya Shetani. Hakunikomboa kwa dhahabu au fedha ila kwa damu yake takatifu pamoja na mateso yake bila kosa na kufa kusudi niwe wake, niishi chini yake katika ufalme wake, na kumtmikia katika haki ya milele bila kosa na heri, kama alivyo fufuka kutoka kwa wafu na anaishi na kutawala pasipo mwisho. Hii ni kweli kabisa.

## FUNGU LA TATU
## UTAKASO

"Na mwamini Roho Mtakatifu, Kanisa takatifu la kikristo, Ushirika wa watakatifu, ondoleo la dhambi, ufufuko wa mwili na uzima wa milele. Amina."

Hii inamaana gani ?

**Jibu** : Naamini ya kwamba kwa akili au kwa nguvu zangu mwenyewe si wezi kumwamini Bwana wangu Yesu Kisto wala kumfikia. Lakini Roho Mtakatifu ameniita kupitia injili, akaniangaza akanipa vipaji vyake na akanitakasa na kunilinda ili nishike imani ya kweli. vivyo hivyo huwaita, uwangaza na kuwatakasa na kuwalinda wakae wakimshika Yesu Kristo ananisamehea mimi pamoja nao wote wamwaminiao dhambi zetu kila siku. Na siku ya mwisho atanifufua pamoja na wafu wote anipe pamoja na wote wa mwaminio uzima wa milele katika Kristo.Hii ni kweli kabisa.

✞ ✞ ✞

## III

## SALA YA BWANA

**Jinsi bwana wa jamaa atakavyofundisha wenzake kwa unyenyekevu wote**

### DIBADJI

**"Baba yetu aliye mbinguni"**

Hii inamaana gani ?

**Jibu** : Hapa Mungu ametuita tuamini ya kuwa yeye ni Baba yetu wa kweli na sisi ni wana wake wa kweli, ili tupate kumfikia kwa ujasiri na kumtegemea kwa maombi kama vile watoto wa mwombwao Baba yao mpendwa.

### OMBI LA KWANZA

**"Jina lako litakaswe"**

Hii ina maana gani ?

**Jibu** : Tuwe na uhakika kwamba jina lake Mungu lenyewe ni takatifu, lakini twaomba katika ombi hili litakaswe hata kwetu pia.

Hii itafanika je ?
Kuwa Neno la Mungu litakaswe kwetu ?

**Jibu** : Wakati Neno la Mungu litafundishwa kwa ku eleweka (ufasaha) na sisi kama wana wa Mungu wapendwa tuishi maisha matakatifu kuligana na neno lake. Ee Baba uliye mbinguni ! Lakini yeyote afundishaye na kuishii vinginevyo zaidi ya Neno la Mungu miongoni mwetu. Katika hili utulinde Baba wa mbunguni !

## OMBI LA NNE

**"Utupe leo riziki yetu ya kila siku"**

Hii inamaana gani ?

**Jibu :** Kuwa na hakika kwamba, Mungu ana wapa watu wote mkate wa kila siku, hata kwa walio wabaya pasipo ombi letu, lakini tu naomba katika ombi hili kuwa Mungu aweze kutufanya tufahamu vipawa vyake na kupokea mkate wetu wakila siku kwa shukrani.

Maana ya mkate wa kila siku ndio nini ?

"Mkate wa kila siku ni"

**Jibu :** Kila kitu kinachohitajika kutosheleza mahitaji ya kimwili, kama chakula na mavazi, nyumba na makao, mashamba na bifugo, fedha na mali, jamaa ya kikristo, na watoto walio wazuri watumishi waaminifu, wotawala wacha Mungu na waaminifu, serikali nzuri, majira ya hali ya hewa, amani na afya, utaratibu na heshima , marafiki wa kweli, majirani waaminifu na mengine yanayofanana na hayo.

## OMBI LA TANO

**"Na utusamehe makosa yetu kama sisi nasi tunavyo wasamehe waliotukosea."**

Hii ina maana gani ?

**Jibu :** tunaomba katika ombi hili kwamba, Baba yetu wa mbinguni asizitazame dhambi zetu, na kwa sababu ya hizo akatae maombi yetu kwani hatuna haki wala vitu hivyo tunavyoomba. Ingawa tuna fanya dhambi kila siku, na hatustahili lolote ila adhabu, hata hivyo sisi tunaomba kwamba yeye Mungu atupe sisi vitu vyote kwa neema yake. Bila shaka sisi kwa upande wetu twasamehe kwa moyo na kwa furaha twatenda mema kwa wale wanaotukosea.

## OMBI LA SITA

**"Na usitutie katika majaribu"**

Hii inamaana ngani ?

**Jibu** : Mungu hamjaribu yeyote kutenda dhambi lakini tunaomba katika ombi hili kwamba Mungu aweza hivyo kutuangalia na kutulinda ili Shetani, dunia na mwili wetu visiweze kutudanganya ao kupotosha, visitutie katika kutokuamini, kukata tamaa na dhambi zingine zenye aibu lakini hata ingawa tunaweza kujaribiwa tunaweza kwa haraka kufaulu na kushinda.

## OMBI LA SABA

**"Lakini utuokoe katika maovu"**

Hii ina maana gani ?

**Jibu** : Tunaomba katika ombi hili kwa kifupi ya kwamba, baba yetu aliye mbinguni anaweza kutuokoa kutoka kwa aina yote ya uovu iwe yenye kuharibu mwili, au moyo, au mali au sifa na mwishowe saa ya kifo aweze kutupa mwisho wenye baraka na kwa neema atuondoe kutoka giza hili la huzuni na atupokee mwenyewe kwake mbinguni hata hivyo sisi tunaomba kwamba yeye Mungu atupe sisi vitu vyote kwa neema yake. Bila shaka sisi kwa upande wetu twasamehe kwa moyo na kwa furaha twatenda mema kwa wale wanaotukosea.

## NA MWISHONI AU KWA KUMALIZA

**"Kwani ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu hata milele. Amina"**

Hii maana gani ?

**Jibu** : Maana yake ni kwamba, nipate kuhakikisha kwa kuwa maombi haya yamekubaliwa na Baba yetu aliye mbinguni na yamesikika naye, kwa kuwa yeye mwenyewe alituagiza tuombe hivi na akatuahidi kutusikia.

"Amina, amina" Maana yake, ndiyo ndivyo iwe hivyo.

✞ ✞ ✞

# IV

# SAKRAMENTI YA UBATIZO

Jinsi Bwana wa jamaa anavyafundisha, wezake na unyenyekevu wote.

## 1. HUU UBATIZO

Ubatizo ni nini ?

**Jibu** : Ubatizo sio maji matupu, bali ni maji yanayo tumika kulingana na amri ya Mungu na kuchanganmana na Neno la Mungu.

Neno hili la Mungu ndio nini ?

**Jibu** : Kama ilivyoandikwa katika Matayo 28 : 19 Bwana wetu Kristo asema « Basi enedeni, - mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa njina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu. »

## 2. FAIDA YA UBATIZO

Ni zawadi au faida gani ubatizo unatoa ?

**Jibu**: Unawezesha msamaha wa dhambi, na kuokoa kutoka mautini na Shetani na kuutoa wokovu wa milele kwa wote wanaoamini, kama Neno na ahadi ya Mungu .

Neno na ahadi ya Mungu hii ndilo nini ?

**Jibu** :Bwana wetu Yesu kristo anasema kutoka injili ya mutakatifu Marko kwa sura yake ya mwisho. "Anaye amini na kubatizwa ataokolewa; asiyeamini atakuhumiwa."

## 3. UKAMILIFU WA UBATIZO

Maji yana wezaje kufanya matendo aya makubwa ?

**Jibu** : Sio maji yenye kufanya matendo, bali ni Neno la Mungu linalochangamana na maji. Kwa kuwa pasipo Neno la Mungu, maji ni maji matupu na sio ubatizo. Lakini wakati yanapochangamana na Neno la Mungu, unakuwa ubatizo ambao ndio maji ya neema kwa maisha, kusafisha na kuhuisha katika Roho Mutakatifu, kama Mtume Paulo alivyo mwandikia Tito 3 : 5 – 8 : "Alituokoa katika kusafishwa na kufanywa upya katika Roho Mtakatifu, ambaye alitumwangia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu, ili tuhesabiwe haki kwa neema yake, tupate kufanywa wariti wa uzima wa milele. Usemi huu ni hakika."

## 4. MAANA YA UBATIZO

Ubatizo una maana gani katika maisha yetu ya kikristo?

**Jibu** : Ubatizo una maana kwamba Adamu wa kale aliye ndani yetu, pamoja na dhambi zote na tamaa mbaya lazima zizamishwe katika uzuni kila siku kwa toba na kuwekwa mbali na kifo, na mtu mpya kuinuka na kutokea kila siku na kuishi milele mbele za Mungu.

Hii imeandikwa wapi ?

**Jibu** : Katika Waroma 6 : 4, Mtume Paulo aliandika : "Basi, tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyo katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi pia twenende katika upya wa uzima."

V

# HUDUMA WA FUNGUO

Jinsi bwana wa jamaa atakavyofundisha walio wake kwa unyenyekevu

## 1. HUDUMA WA FUNGUO

Huduma wa funguo ni nini ?

Ni uwezo wa kipekee Bwana Yesu Kristo aliyotoa kwa kanisa duniani. Anawasamehe wenye dhambi na wenye kuomba musamaha na kukataa kuwasamehe wasioadibishwa, wakati wowote wanapo fanya mioyo yao kuwa mugumu.

Imeandikwa wapi ?

Imeandikwa kutoka injili ya Mutakatifu Yoane , sura yake 20:23 : "Yesu Kristo akapuliza juu yao, akawambia : Mpokee Roho Mtakatifu, wowote mutakao wasamehe dhambi, zinasamehewa kwao, na wale musiosamehe hawatasamehewa."

## 2. MATUMIZI YA HUDUMA WA FUNGUO

Unaamini nini kuhusu huduma wa funguo kufatana na Neno la kawaida?

Na amini ya kwamba wa tumishi wa Kristo, wanaitwa kwa huduma Mutakatifu kufanya kazi kati yetu panafasi ya Yesu kupitiya kwa ruhusa ya Mungu. Waki ifanya kufuatana na Neno la Mungu, hiyo itakuwa na bei, hata mbinguni, ni kama Bwana wetu Yesu Kristo alivyo ifanya mwenyewe. Hakika kwa upekee wanapotenga katika jamii ya kikristo waovu na wenye kukataa kuungama. Ni hakika pia wanapo samehe dhambi kwa wanao tubu na wenye kuhaidi mabadiriko ya mwenendo wao.

### 3. KUKIRI NA UTAKASO

Kukiri ni nini ?

Kukiri kuna maana mbili: kwanza, kukubali dhambi. Pili, kupokea toka mchungaji msamaha wa dhambi kama vile musamaha wa dhambi ni kutoka kwa Mungu mwenyewe na kukubali bila shaka lolote yakama dhambi imeondolewa mbele ya Mungu.

### 4. NI DHAMBI GANI ZA KUTUBU

Ni dhambi gani tunapashwa kutubu?

Mbele ya Mungu tunapashwa kutubu dhambi zote, hata dhambi tusizofahamu, kama tunavyo omba katika sala ya Baba yetu. Kwa lakini kwa mchugaji tunatubu dhambi zile tunazofahamu na zinazotulemea kaika zamiri zetu.

Ni dhambi gani?

Tazama hali yako, kufatana na Amri kumi, ukiwa baba, mama au mtoto, bwana au mutumishi. Chunguza mwenendo wako. Ujiulize kama ulikuwa muasi, mpagano au muzembe, kama ulikosea au uliuzunisha mtu kwa maneno au kwa matendo; kama uliiba kitu chochote hicho au uliharibu kwa kupuusa kwako, kwa kukosa namna yoyote na utaratibu.

✞ ✞ ✞

## SAKRAMENTI YA MADHABAHU AO MEZA YA BWANA

Jinsi Bwana wa jamaa wanavyopaswa kuwafundisha walio wake kwa unyenyekevu.

1. Sakramenti ya Meza ya Bwana ni nini?

**Jibu:** Sakramenti ya Meza ya Bwana ni mwili na damu ya kweli ya Bwana wetu Yesu Kristo katika mkate na divai, iliyoanzishwa na Kristo mwenyewe kwa ajili yetu wakristo katika kula na kunywa.

Hayo yameandikwa wapi?

**Jibu** : Wainjilisti watakatifu Matayo, Marko, Luka na pia Paulo Mtakatifu wanaandika hivi: "Bwana wetu Yesu Kristo usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega akawapa wanafunzi wake, akisema: Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu uliotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu." Na vivi hivi baada ya kula akakitwa kikombe, akawapa, akisema: "Nyweni nyote katika hiki. Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano jipya, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondolea la dhambi. Fanyeni hivi, kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu."

**1. Neema ya meza ya Bwana ni nini?**

**Jibu:** Tunaonyeshwa na maneno haya: Imetolewa kwa ajili yenu damu imwagikayo kwa ondoleo la dhambi. Naam, kwa maneno haya katika sakramenti tunapata msamaha wa dhambi, uzima na haki. Kunako msamaha wa dhambi, kuna pia uzima na haki.

**2. Inatoka wapi neema ya Meza ya Bwana au ushirika mtakatifu?**

**Jibu:** Aiko kula na kunywa pekee yake kwaweza kutenda mambo haya, lakini maneno haya kwa ajili yenu na imwagikayo kwa ondoleo la dhambi yanayoambatana nayo. Maneno haya ni mbali ya kula na kunywa kimwili

" Tiini wenye kuwaongoza ninyi na kuwanyenyekea; maana wao wanaangalia kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili
na ndiyo mambo makuu katika sakramenti. Anayeamini maneno haya kadiri yanavyosema, na yanavyosikia, atajipatia msamaha wa dhambi.

**3. Ni nani anayepokea sakramenі hii kwa ustahifu?**

**Jibu**: Kufunga na kujitayarisha kimwili ni mazoezi mazuri ya nje, lakini ayaaminiye maneno haya: kwa ajili yenu na imwagikayo kwa ondoleo la dhambi, yeye ndiye anayestahili kwa kuwa maneno haya kwa ajili yenu yanakuwa faraja ya mioyo inayoamini kweli.

✞✞✞

## JINSI BWANA WA JAMAA ATAKAVYOFUNDISHA WENZAKE KUSEMA SALA ZA ASUBUHI NA MAGHARIBI

Ona mfano ya maombi mbilimbili wanaweza kutumia asubui na magharibi.
SALA YA ASUBUI
Asubui unapoamka asubui unaweza kuomba hivi: Kwa jina la Baba na la Mwana na Roho Mtakatifu. Amina.

Halafu, ukiwa umpiga magoti au umesimama, useme Ukiri wa Mitume na Sala ya Bwana. Kisha unaweza kusema sala hii fupi:
"Nakushukuru wewe Baba wa mbinguni kwa Mwana wako mpendwa Yesu Kristo, kwa kuwa umenilinda usiku huu juu ya maumivu yote na hatari zote. Nakusihi ukitaka unilinde pia siku hii ya leo dhidi ya dhambi na uovu wote, ili matendo yangu na maisha yangu yote yaweze kukupendeza. Mikononi mwako na kabidhi mwili wangu na roho yangu na vyote ili yule Ibilisi asiweze kuwa na uwezo wowote juu yangu. Amina."

**Kisha uenda kazini mwako na furaha ukiimba wimbo.**

SALA YA MAGHARIBI : magharibi unapokwenda kulala,Omba hivi: " Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina."

**Halafu, ukiwa umepiga magoti au umesimama useme Ukiri wa Mitume na Sala ya Bwana. Kisha, utaweza kusema sala hii fupi ukipata nafasi:**

"Nakushukuru wewe Baba wa mbinguni kwa Mwana wako mpendwa, Yesu Kristo, kwa kuwa umenilinda siku hii kwa huruma yako. Nakushihi kwamba ukitaka unisamehe dhambi zangu zote kadiri nilivyotenda makosa, na unilinde usiku huu kwa huruma yako. Mikononi mwako nakabidhi mwili wangu na roho yangu na vyote nilivyonanavyo. Malaika wako matakatifu awe pamoja nami ili yule Ibilisi asiweze kuwa na uwezo wowote juu yangu. Amina."

**Kisha unapaswa kulala salama pasipo woga**

## JINSI BWANA WA JAMAA WANAVYOPASWA KUWAFUNDISHA WALIO WAKE KUBARIKI NA KUSHUKURU KABLA NA BAADA YA KUTUMIA CHAKULA

Kabla ya chakula

Jinsi Bwana wa jamaa anavyopaswa kufundisha wenzake kubariki na kushukuru kabla ya chakula.
Inawabidi wote walioino nyumbani kuketi mezani kwa hali ya ulilivu na kushikamanisha mikono yao na kusema: " Macho ya watu wote yanakuelekea wewe, ee Bwana, nawe huwapa chakula chao wakati wake. Waufumbua mkomo wako, wakishibisha kila kilicho hai kwa baraka yako. (Mameno haya imetoka kwa kitabu cha Zaburi 104: 27 –28)

Halafu Sala ya Bwana isemwe na kisha ombi hili:

"Bwana Mungu Baba wa mbinguni utubariki na vipaji vyoko ulivyotupa, tuvitumie kwa ukarimu wako, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amina."

Baada ya chakula wakati wanapo maliza kwakutumia chakula, kushikamanisha mikononi kwamba: "Mshukuruni Bwana Kwa kuwa yeye ni mwema, kwa maana rehema yake ni ya milele,anamupa nyama chakula chake, na wana-kunguru wanaolia: Hafurahii nguvu ya farasi hapendezwi na miguu ya mtu.. Bwana anapedenzwa nao wanaomwogopa, Nao wanaotarajia rehema. kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amina."

Halafu sala ya Bwana isemwe kisha ombi hili: "Tunakushurkuru Bwana Mungu, Baba yetu kwa rehema zako zote, Kwa Yesu Kristo Bwana wetu aishiye na kutawala milele na milele. Amena."

ñ

## UTARATIBU WA NYUMBANI

**Jinsi Biblia Inafundisha kufatana na wajibu ya wa watu wa kwachana.**

## WAJIBU WA VIOGOZI WA KANISA

Wajibu wakiongozi wa kanisa. Imempasa awe mtu asiye laumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu mkaribishaji, ajuaje kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana; wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu….Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu nk….(1 Tim.3: 2 – 6); Tite 1: 6 – 9

## WAJIBU WA WAMINIFU KWA WALIMU NA WA WACHUNGAJI

"Kaeni Katika nyumba ile, mukikula na
kunywa vitu munavyopewa kwao kwa maana mutenda kazi anastahili kupewa mushahara wake. Musihame nyumba kwa nyumba." (Luka 10: 7)
"Hivi Bwana aliagiza ya kwamba wale wanao hubiri habari jema wapate, maisha yao kwa habari jenma." (1 Wakorinto 9: 14 )

" Lakini yeye aliyefundishwa katika neno, ashiriki naye aliyefundisha katika maneno yote yaliyo mema. Musidanganywe: Mungu hazikiwi; yo yote mutu anayopanda, ndiyo atakayovuna"(Wagalatia 6: 6 – 7)

"Wazee wanaotawala vema wahesabiwe kustahili heshima mara mbili, zaidi wale wenye kujitaabisha sana kwa neno na kwa mafundisho. Kwa sababu madiko yanasema usfunge kinywa cha ngombe wakati anapo kanyanga ngano; na tena; Mutenda kazi anastahili mushara wake." (1 Timoteo 5: 17 – 18)
" Lakini tunawasihi ninyi, ndugu, mujue wale wanaosumbuka sana katikati yenu, na kuwasimamia ninyi katika Bwana, na kuwaonya ninyi; na muwaheshimu sana katika mapendo kwa ajili ya kazi yao. Muwe na salama katikati yenu." (1 Watesalonika 5: 12 – 13)

wapate kufanya hivi kwa furaha, wala si kwa huruni: maana hii itakuwa kwenu pasipo faida." (Waebrania 13: 17)

**KUHUSU SEREKALI**

Kila mutu atii wakubwa wenye amri: kwa maana hapana mamlaka ila kwa Mungu: na mamlaka inayokuwa, imeweka na Mungu. Hivyo yeye anayeshindana na mwenye mamlaka, anashindana na amri ya Mungu; nao, waoshindana watajipatia hukumu. Kwa maana watawala hawaleti watu woga kwa matendo mema, lakini kwa matendo mabaya. Basi unataka usiogope mwenye mamlaka? Fanya mema, na utapata sifa kwake; kwa kuwa yeye ni mutumishi wa Mungu kwako kwa mema. Lakini wakati unapofanya mabaya, ogopa; kwa sababu habebi upanga bule: maana ni mutumishi wa Mungu anayelipiza kisasi mwenye kufanya mabaya." (Waroma 13: 1.2-4)

**KWA WANAINCHI**

Kwa hivyo ni sharti kutii, si kwa sababu ya gazabu tu, lakini kwa sababu ya zamiri vilevile. Kwa sababu hii tena mulipe kodi; kwa kuwa wao ni watumishi wa kazi ya Mungu, wakidumu katika kazi hii. Muwape wote haki zao; mutu wa kodi, kodi; mutu wa ushuru, ushuru; mwenye kustahili woga; woga; mwenye kustahili heshima, heshima."(Waroma 13: 5-7)

"Neno hili ni la kweli: Kwama mutu akitaka kazi ya mwangalizi, anataka kazi nzuri. Basi imemupasa mwangalizi asiwe na laumu, mume wa muke mumoja, mwenye kiasi, mwenye akili, mutu wa utaratibu, mukaribishaji wageni, mwenye kujua kufundisha; si mutu wa kulewa na mvinyo, si mupiganji, si mwenye tamaa ya feza; lakini awe mupole, si mutu wa ugomvi, asiwe mwenye kutamani." (1 Timoteo 2: 1 –3)

"Ukumbushe watu kunyenyekea wenye kutawala na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari, kwa kila kazi njema." (Tito 3:1)

"Tukitazamia tumaini la baraka, na kuonekana kwa utukufu wa Mungu mukubwa, Mwokozi wetu Yesu Kristo : aliyejitoa mwenyewe kwa ajili yetu atumboe toka uovu wote, na kujisafisha watu wawe mali yake mwenyewe, wenye bidii sana katika kazi njema."(1 Petro 2: 13 – 14)

## WAJIBU YA WAUME KWA WAKE ZAO

"Tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa wariti kwa tumaini la uzima wa milele." (1 Petro 3:7)
"Waume, mupende wake wenu, wala musiwe na uchungu nao." (Wakolosayi 3: 19)

## WAJIBU YA WAKE KWA WA UME ZAO

"Ninyi wake, mutii waume wenu, kama kutii Bwana." (Waefeso 5: 22)

"Kama Sara alivyotii Abrahamu akimwita bwana; nanyi ni watoto wake kama mukifanya mema wala hamwogopeshwi kwa woga wo wote."(1 Petro 3: 6)

## WAJIBU YA WAZAZI KWA WA TOTO

" Baba, musichokoze watoto wenu, wasichoke katika roho zao. Nanyi baba, musichokoze watoto wenu; lakini muwalee katika azabu na maonyo ya Bwana."(Wakolosayi 3: 21; Waefeso 6: 4)

## WAJIBU YA WATOTO KWA WAZAZI

"Watoto, mutii wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Heshimu baba yako na mama yako (hii ni amri ya kwanza yenye ahadi) upate heri, na uishi siku nyingi katika dunia."(Waefeso 6: 1- 3)

## WAJIBU WA WATUMISHI, MABWANA WA TENDA KAZI WAO

"Watumwa, mutii wao walio bwana zenu kwa maneno ya mwili, kwa woga na kutetemeka, kwa roho moja, kama kutii Kristo; si kwa utumwa wa macho tu, kama wenye kupendeza watu; lakini kama watumwa wa Kristo, mukifanya mapenzi ya Mungu kwa moyo; kwa nia njema kama kutumikia Bwana, wala si watu; mukijua ya kuwa kila neno jema mutu analotenda, atalipata tena toka Bwana, kama yeye ni mutumwa ao kama ni huru. "(Waefeso 6: 5-8)

## WAJIBU WA MABWANA KWA WA TENDA KAZI WAO

"Na ninyi bwana, muwatendee hivi vilevile, mukiacha kuwaogopesha; mukijua ya kuwa yeye aliye Bwana wao na wenu ni mbinguni wala kwake hakuna upendeo."(Waefeso 6: 9 )

"Kaeni katika nyumba ile, mukikula na kunywa vitu munavyopewa kwao; kwa maana mutenda kazi anastahili kupewa mushahara wake "(Luka 10: 7 )

## WAJIBU WA VIJANA KWA WAZEE

" Mujinyenyekeze basi chini ya mukono wa uwezo wa Mungu, ili awatukuze ninyi kwa wakati wake."(1 Petro 5: 6)

## WAJIBU WA WAJANE

"Lakini yeye aliyefuata tamaa zake amekwisha kufa angali yeye ni hai. " (1 Timoteo 5: 6 )

## WAJIBU WA WAKRISTO

"Maana yake, Usizini, Usiue, Usiibe, Usisihuhudu uwongo, Usitamani; na kama ikiwa amri nyingine yo yote, inajumlika katika neno hili, Penda jirani yako kama wewe mwenyewe " (Waroma 13: 9)

"Basi ninaonya mbele ya maneno yote, kuomba, na kusihi, na kuombea, na kushukuru kufanyike kwa ajili ya watu wote " (1 Timoteo 2: 1)

**Ama mutu yeyote anajifunza masomo haya,yote itakuwa vema nyumbani.**

# MFANO WA UCHUNGUZI WA ZAMIRI

## ILIYOPEDEKEZWA NA DK MARTIN LUTHER KWA WALE WANA HURUSIWA KULA CHAKULA CHA BWANA.

Mbele ya kula chakula cha Bwana, kila mwaminifu anaitajiwa kufundishwa Amri Kumi ya Mungu ; imani ya kikristo, Baba yetu, ubatizo na ushirika wa meza ya Bwana.

Baada ya madifunzo, mchungaji anaweza kuwa uliza maswali na kuwajaribu ndani ya kanisa, na wana weza kujibu kwa maswali hiyo mwaminifu au mkristo ana weza kujijaribu mwenyewe kufatana na mashauri ya mtume Paulo kwa 1 Korinto 11 : 28-29.

1. **Unaamini ya kwamba uko mtenda dhambi ?**
   Ndiyo, ninaamini ya kwamba niko mwenye dhambi.

2. **Unajuwa mfano gani ?**
   Neno la Mungu linanifundisha ya kama si kutii Amri kumi ya Mungu.

3. **Una nungunika kwa dhambi yako ?**
   Ndiyo, nina ningunika kwa kuweza kumkoseya Mungu.

4. **Unastahili nini mbele ya Mungu kwa dhambi yako ?**
   Nimestahili hasira ya Mungu na azabu kwa haki ya mwenyezi. Ninastahili mwenyewe kifo hapa duniani na hukumu ya milele ni ile mutume paulo anaandika.
   "Basi faida gani muliyopata kwa maneno yale munayo yaona haya juu yao sasa ? Kwa maana mwisho wa maneno haya nikufa. Lakini sasa mukikwisha kuwekwa huru toka dhambi, na kufanyua watumwa wa Mungu, faida munayopata nikutakaswa, na mwisho wake uzima wa milele. Kwa maana mushahara wa dhambi ni mauti, lakini zawadi ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana yetu". (Waroma 6 : 21-23)

5. **Unatumaini kuokolewa ?**
   Ndiyo, ninatumaini kweli kabisa.

6. **Unaweka tumaini kwa nani ?**
   Ninaweka tumaini yangu kwa kristo Yesu Bwana wangu.

7. **Yesu Kristo ni nani ?**
   Ni mwana wa Mungu. Tena ni Mungu wa kweli na mwanadamu wa kweli.

8. **Kuna miungu migapi ?**
   Kuna Mungu moja tu, katika utatu : Baba, Mwana, na Roho mtakatifu.

9. **Nini Yesu Kristo alikufanizia, upate kumutumaini ?**
   Alikuja na alimwanga damu ku musalaba kwa ajili ya dhambi hili nipate musamaha wa dhambi zangu.

10. **Je Mungu baba naye alikufa kwa ajili yako?**
    Hapana, Mungu Baba ni Mungu mwenyezi, Roho mtakatifu naye ni Mungu. Kwa lakini Mwana yeye ni Mungu wa kweli tena mwanadamu wa kweli. Aliyekufa na liyemwanga damu kwa ajili yangu.

11. **Unajuwa je kama Yesu alikufa kwa ajili yako ?**
    Nilijifunza katika neno la Mungu. Ndani ya Neno la kawaida ya chakula cha Bwana na ushirika mutakatifu.

12. **Ni mapendo gani ya kawaida ya chakula cha Bwana ?**
    "Bwana wetu Yesu Kristo, usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, akamshukuru Mungu, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akisema: Twaeni mle, huu ndio mwili wangu uliotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi.
    Vivyo hivyo baada ya kula akatwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akasema : twaeni nyweni nyote katika hiki kwa maana kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu inayomwangika kwa ajili yenu na kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. Fanyeni hivi kila mara munapokunywa kwa kunikumbuka."

13. **Unaamini kuwa katika meza ya bwana unaupokea kweli mwili wa kweli na damu ya kweli ya kristo?**
    Divyo naamini kweli.

**14. Tumaini yako ina msingi wapi ?**

Tumaini yangu lina msingi katika neno la Yesu: "Twaeni mle, huu ndio mwili wangu… nyweni wote, hii ni damu yangu."

**15. Tutafanya nini wakati tunapo kula mwili wake na kunwa damu yake, kwa ajili ya ukombozi ?**

Tunapashwa kutangaza kifo na kujitao kwa Bwana Yesu iwe ukumbusho kwake, kama alivyotu amuru "Fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu."

**16. Kwanini tunaweza kutangaza kifo chake na kuikumbuka ?**

Tunakumbuka kifo cha Yesu, tupate kujifunza na kuamini ya kwamba hakuna kiumbe chochote kiliweza kulipa zambi zetu, ila tu Yesu Kristo yeye ni Mungu wa kweli na mwanadamu wa kweli.

Tunapashwa ku kumbuka kifo cha Yesu, tupate kujifunza na kwangaliya dhambi kwa woga na kutazamia kama kuto kutii ni kosa kubwa.

Imetupasa kumbuka kifo cha Yesu, kwa kupata furaha na salama yetu ndani mwake yeye na kuokolewa katika imani hii.

**17. Nini iliyomusukuma yesu afe kwa ajili ya dhambi. zako, ili awalipie ?**

Ni upendo kubwa wa Yesu kwa Baba yake, juu yangu na kwa wote wakosefu, aliyojitoa afe kwa ajili ya dhambi zangu. Ona ilivyoandikwa ndani ya Biblia :

" Hakuna mwenye mapendo kuliko haya, mutu kutoa uzima wake kwa sababu ya rafiki zake." (Yoane 15 : 13)

" Lakini Mungu anaonyesha mapendo yake kwetu, wakati tulipokuwa tungali wenye dhambi,Kristo alikufa kwa ajili yetu." (Waroma 5 : 8)

" Nimesulubiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai ; wala si mimi, lakini Kristo ni hai ndani yangu ; na uzima nilio nao sasa katika mwili, ni uzima wa imani iliyo ya Mwana wa Mungu aliyenipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." (Wagalatia 2 : 20)

" Na mutembee katika mapendo, kama Kristo vilevile alilvyowapenda ninyi na kujitoa mwenyewe kwa ajili yetu, toleo na zabihu kwa Mungu kuwa harufu ya manukato." (Waefeso 5 : 2)

**18. Kwanini unatumaini kushiriki chakula cha Bwana ?**

Na tumaini kushiriki chakula cha Bwana kwa kujifunza kwakwamini ya kwamba Yesu, ndani ya upendo, alikufa kwa ajili yangu, kwa sababu ya dhambi zangu, na kuwa na uhakika wa musamaha, nami tajifunza kwake kumupenda Mungu na jirani yangu.

**19. Kwa sababu gani muaminifu anatamani kushirikl meza ya Bwana ?**

Kwanza Bwana wetu alivyomwamuru na akamuongezea ahadi. Ndiyo sababu ya kwanza. Kwakuwa kuna taabu ya dhambi zetu ambayoinatupasa kushiriki. Nikwasababu ya taabu hiyo, Bwana Yesu anatuwamuru kwenda kushiriki meza ya Bwana , anatuita na kutuaidia.

**20. Kama mutu hapati taabu na kuwa na njaa na kiu ya meza takatifu, atafanya nini ?**

Inapashwa kwanza ku mwambia, apate kujichunguza kuona kama yeye ni mkristo kweli. Na baadaye akumbuke namna Biblia inavyosema juu ya mtu.

" Basi matendo ya mwili yanaonekana, ndiyo : uasherati, uchafu, uzinzi, kuabudu sanamu, ulozi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, uuaji wa mutu, ulevi, ulafi, na yanayofanana na maneno haya ; juu ya maneno haya ninawaambia ninyi mbele kama nilivyowaambia ninyi zamani ; watu wale wanaotenda maneno ya namna hii, hawatariti ufalme wa Mungu." (Wagalatia 5 : 19-21)

"Kwa maana ninajua ya kwamba ndani yangu, maana, ndani ya mwili wangu, halikai neno njema ; kwa sababu kutaka ni kwangu, lakini kufanya lililo njema siwezi." (Waroma 7 : 18)

Pili, aone kwanza kando kando yake, atazame tena kama angali tu katika dunia inamupasa kwanza ajuwe namna inavyofundishwa katika Biblia, dhambi aitakosa kamwe duniani.

"Kama dunia ikiwachukia ninyi, munajua ya kama ilinichukia mimi mbele ya kuwachukia ninyi. Kama mungekuwa wa dunia, dunia ingependa watu wake ; lakini kwa sababu ninyi si wa dunia, lakini nimewachagua ninyi toka dunia, kwa sababu hii dunia inawachukia ninyi." (Yoane 15 : 18-19)
"Kweli, kweli ninawaambia ninyi, mutalia na kuomboleza, lakini dunia itafurahi; na ninyi mutakuwa na uzuni, lakini uzuni yenu itangeuka kuwa furaha." (Yoane 16:20)
"Musipende dunia, wala maneno kati dunia. Mtu akipenda dunia , mapendo ya Baba si ndani yake. Maana kila kitu kilicho katika dunia, na tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitoki kwa Baba lakini vinatoka kwa dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zako, lakini yeye anayefanya mapenzi ya Mungu anadumu hata milele."(Yoane 2:15-17)

"Unajua ya kuwa kila mutu alizaliwa na Mungu hatendi dhambi; lakini yeye aliyezaliwa na Mungu anajilinda mwenyewe, wala yule mwovu hamugusi."(1Yoane 5: 18)

Tatu, anapashwa kufahamu ya kama shetani anzunguka kando kando yake usiku na mchana. akiwa na uongo pia na makali, Shetani hawezi kumuacha akae katika salama. Atakuwa na kikwazo ndani ya moyo wake na ndani ya maisha yake, ndivyo Biblia inavyotufudisha.
Ninyi wa baba yenu Shetani na tamaa za baba yenu manataka kuzifanya. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, na hakukaa katika kweli ; kwa sababu hakuna kweli ndani yake. Wakati anaposema uwongo, anasema yaliyo yake mwenyewe, kwa sababu yeye ni muwongo, na baba ya wongo." (Yoane 8 : 44)

"Muwe na kiasi na kuangalia ; adui yenu Shetani, kama simba anaye unguruma anazungukazunguka akitafuta mutu amumeze. Nanyi mushindane naye katika imani yenu, mukijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walio duniani." (1 Petelo 5 : 8 – 9)

"Vaeni silaha zote za Mungu, mupate kuweza kusimama juu ya hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama, lakini juu ya ufalme na mamlaka, juu ya watawala wa ulimwengu wa giza hili, juu ya majesi ya pepo wabaya katika pahali pa mbingu." (Waefeso 6 : 11-12)

"Akiwaonya kwa upole wenye kushindana naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awape kutubu na kujua kweli, na wapate tena akili zao na kutoka katika mutego wa shetani, waliofungwa naye, kufanya mapenzi yake." (2 Timoteo 2 : 25-26)

## MAFAFANUZI

Maswali na majibu hayo, haiko mchezo wa watoto. DK Martin Luther alikuwa na mukazo wakati alipowaandikia na nia ya kuwasaidia vijana na wazee kwa kujichunguza mbele ya kula chakula cha Bwana. Yote yapatikana katika Neno la Mungu na Paulo anasema :
"Musidanganywe : Mungu hazihakiwi ; yo yote mutu anayopanda, ndiyo atakayovuna." (Wagalatia 6 : 7)

✞✞✞

# MAELEZO KUHUSU KATEKISIMO NDOGO YA MARTIN LUTHER

## UTANGULIZI

1. **Kitabu tutakacho jifunda kinaitwa je?**
   Kinaitwa katekisimo.
2. **Katekisimo ni nini?**

Katekisimo ni kitabu cha maadibisho ya kidini kwa njia ya maulizo na majibu. Karibu kila mara inasindikizwa na haya za Biblia ili kuthibitisha kama majibu inatokana na Neno la Mungu. Mwisho wa haya, kuna "anuani" au maelekezo. Zinatuonyesha wapi zinapatikana ndani ya Biblia. Kwa mfano, 2 Petro 1: 21 inaonyesha kama haya hii hupatikana katika waraka wa pili wa Petro sura ya kwanza na mustari wa 21.

3. **Nani aliye andika katekisimo ndogo tunayo jifunza?**
   Ni Martin Luther, mutengenezaji wa kanisa aliye andika katekismo ndogo mwaka 1529. Luther amezaliwa tarehe 10 mwezi wa november mwaka 1483 na amefariki tarehe 18 february 1546.
4. **Katekisimo ndogo inatufundisha nini?**
   Katekisimo ndogo utufundisha mambo ya muhimu ya dini la kikristo. Inaeleza kweli iliyo ya lazima sana yenye kufundishwa ndani ya Biblia.
5. **Ni mambo gani ya muhimu ya dini ya kikristo?**
   Ni pointi sita zifwatazo:
   1) Amri kumi( Torati au sheria).
   2) Imani ya kikristo (Imani au alama za mitume).
   3) Baba yetu (otuba wa jumapili).
   4) Sakramenti ya ubatizo takatifu.
   5) Uduma wa funguo na ukiri.
   6) Ushirika wa meza ya Bwana au meza takatifu.
6. **Martin Luther alizipata wapi zile mambo za muhimu za dini ya kikristo?**
   Martin Luther amezipata ndani ya Biblia. Ona swali la pili.

**BIBLIA**

7. **Biblia ni nini?**
Biblia ni kitabu kinacho tufunulia Neno la Mungu. Inaitwa pia:
Biblia takatifu
Maandiko takatifu
Maandiko
Andiko
Ingawa jina wanalotoa kwa Biblia, ni Neno la Mungu siku zote. Ina gawanyika kwa vipande viwili: agano la kale na agano jipia. Na zaidi yake kila agano ina wingi fulani wa vitabu. Mtakuta majina ya vitabu hivyo mwinsho wa katekisimo hii.
8. **Nl nani aliye andika Biblia?**
Kuna watu waliyochaguliwa na Mungu ili kuandika neno lake. Manabii waliandika agano la kale na mitume wakaandika vitabu vya agano jipya. Shikeni kwamba agano la kale liliandikwa katika lugha ya kiebrania na agano jipya katika lugha ya kiyunani.

   1. Siyo kwa mapenzi ya mwanadamu unabii ulitolewa, bali ni kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu watu walinena kutoka kwa Mungu (2 Petro1: 21).

9. **Tunasema kama Biblia ili andikwa na watu. Twaweza je kusema basi kama ni Neno la Mungu?**

   2. Kila andiko linapumzi ya Mungu na linafaa kwa kufundisha (2 Timoteo 3: 16)

10. **"Andiko lina pumzi ya Mungu" maana yake nini?**
Hili neno linamaanisha kuwa Mungu Roho Mtakatifu alisukuma awa watu kuandika. Aliwapa mawazo waliyo eleza na maneno yenye kufaa wakatende hivyo. Hii inaitwa uvuvio yenye uwezo au Kamili ya Biblia.
   3. Siyo kwa mapenzi ya wanadamu unabii hata mmoja ulitolewa, bali ni kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu wanadamu wakisema yalitoka kwa Mungu (2 Petro 1: 21)

4. Tunayasema, si kwa hotuba ifundishwayo na hekima ya wanadamu, bali na ile ifundishayo roho, kwa kueleza ukweli wa kiroho kwa watu wakiroho (1Wakorinto 2: 13).

6. **Maneno yote ya Biblia inatoka kwa nani?**
Maneno yote ya Biblia ni ya Mungu. Ni kwasababu hiyo tunasema hamna kosa lolote ndani ya Biblia .Kila kintu kinaposemwa ndani ya Biblia kimevuviwa na kimetoka kwa Mungu.
   1. Uwatakase kwa kweli; neno lako ni kweli. (Yoane 17: 17)
   2. Kila andiko limevuviwa na Mungu, na linafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki (2 Timoteo 3:16)
   3. Maandiko hayawezi kuvunjika (Yoane 10: 35)

7. **Kwanini Mungu ametupa Biblia?**
Mungu ametupata Biblia ili tuokolewe kwa njia ya imani ndani ya Yesu Kristo.
   4. Tangu utoto wako umejua maandiko matakatifu; yanaweza kukupa hekima, ili upate wokovu kwa imani ndani ya Kristo Yesu. Kila andiko limevuviwa na Mungu, na linafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki ili mtu wa Mungu awe mukamilifu, ametengenezwa kabisa kwa kuwa tendo njema. (2 Timoteo 3: 17)
   5. Neno lako ni taa kwa miguu yangu, na nuru kwa njia yangu.(Zaburi 119: 105)

8. **Twaweza je kutumia Biblia?**
Tunapashwa kulisoma na kujifunza kwa heshima .Kwa hiyo,Tunaweza kusikiya pia yale anayotufundisha. Mwishowe, tuweke tumaini letu kwa yale anayosema na kuishi kufatana na mafundisho.

   6. Munatafuta katika maandiko, kwa sababu munazania ya kuwa ndani yao munauzima wa milele; na maandiko haya ndiyo yanayonishuhudia (Yoane 5: 39)
   7. Lakini yeye alisema: Afazali heri wale wenye kusikia Neno la Mungu na kulishika.(Luka 11: 28)
   8. Lakini Maria akashika maneno haya yote, akayafikiri kwa moyo wake. (Luka 2:19)

13. Yesu akajibu, akamwambia : Kama mutu akinipenda, atatii neno langu, na Baba yangu atamupenda, nasi tutakuja kwake, na tutafanya makao yetu kwako (Yoane 14: 23)
Mara ingine wanatumia katika mafundisho ya dini, ya "Historia takatifu." Ni vitabu vinavyo eleza adisi za Biblia. Inasaidia kwelewa vizuri somo ambayo tumejifunza na hivi ina imarisha imani.

## HISTORIA TAKATIFU

Matendo 17: 10 – 15: Mtume Paulo alitangaza habari njema ya Yesu. Siku moja aki fundisha Beroya, waamini wakafungua Bibla ili kuhakikisha kama aliyo waeleza ni kweli na inaambatana na neno la Mungu.

Matendo 8: 26 – 40 : Filipo alitumwa na Roho Mtakatifu kwaajili ya kumweleza Neno la Mungu , mtu moja mwenye mamlaka wa ethiopia.

## SHERIA NA INJILI

4. **NI mafundisho gani makuu mbili ndani ya Biblia ?**
Mafundisho mbili makuu ndani ya Biblia ni
Torati na Injili.

5. **Mungu hanatufundisha nini katika Torati?**
Katika Torati, Mungu anatufundisha jinsi tunavyo pashwa kuwa na jinsi tunapashwa kuenenda . Anatueleza tuwezayo kufanya au yale tusioweza kufanya.

14. Bwana akamwambia Musa akisema: Sema na makutano yote ya wana wa Israeli na kuwaambia: Mutakuwa watakatifu kwa sababu mimi Bwana Mungu wenu ni mutakatifu.(Walawi 19: 1- 2)
15. Angalia neno hili ninalokuwamuru leo; tazama, ninafukuza mbele yako Muamori, na mukanana, na Muuhiti na muperizi, na Muhivi, na Muyebusi.(Kutoka 34: 11)

Na maneno haya ninayo kuagiza leo, yatakuwa katika moyo wako; na utayafundisha kwa watoto wako kwa bidii, na kusema juu yao wakati unapo keti nyumbani mwako, na wakati unapo tembea

"Kwa maana ninajua ya kwamba ndani yangu, maana, ndani ya mwili wangu, halikai neno njema ; kwa sababu kutaka ni kwangu, lakini kufanya lililo njema siwezi." (Waroma 7 : 18)

Pili, aone kwanza kando kando yake, atazame tena kama angali tu katika dunia inamupasa kwanza ajuwe namna inavyofundishwa katika Biblia, dhambi aitakosa kamwe duniani.

"Kama dunia ikiwachukia ninyi, munajua ya kama ilinichukia mimi mbele ya kuwachukia ninyi. Kama mungekuwa wa dunia, dunia ingependa watu wake ; lakini kwa sababu ninyi si wa dunia, lakini nimewachagua ninyi toka dunia, kwa sababu hii dunia inawachukia ninyi." (Yoane 15 : 18-19)
"Kweli, kweli ninawaambia ninyi, mutalia na kuomboleza, lakini dunia itafurahi; na ninyi mutakuwa na uzuni, lakini uzuni yenu itangeuka kuwa furaha." (Yoane 16:20)
"Musipende dunia, wala maneno kati dunia. Mtu akipenda dunia , mapendo ya Baba si ndani yake. Maana kila kutu kilicho katika dunia, na tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitoki kwa Baba lakini vinatoka kwa dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zaka, lakini yeye anayefanya mapenzi ya Mungu anadumu hata milele."(Yoane 2:15-17)

"Unajua ya kuwa kila mutu alizaliwa na Mungu hatendi zambi; lakini yeye aliyezaliwa na Mungu anajilinda mwenyewe, wala yule mwovu hamugusi."(1Yoane 5: 18)

Tatu, anapashwa kufahamu ya kama shetani anzunguka kando kando yake usiku na mchana akiwa na uongo pia na makali, shetani hawezi kumucha akae katika salama. Atakuwa na kikwazo ndani ya moyo wake na ndani ya maisha yake, ndivyo Biblia inavyotufudisha.
Ninyi wa baba yenu Shetani na tamaa za baba yenu manataka kuzifanya. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, na hakukaa katika kweli ; kwa sababu hakuna kweli ndani yake. Wakati anaposema uwongo, anasema yaliyo yake mwenyewe, kwa sababu yeye ni muwongo, na baba ya wongo." (Yoane 8 : 44)

**17. Mungu anatueleza nini katika Injili?**

Katika Injili, Mungu anatupasha habari njema ya wokovu wetu ndani ya Kristo. Habari njema hii inafunuliwa katika Biblia tu.

18. Kwa hivi mapendo ya Mungu yanaonekana kwetu, kwakuwa Mungu amemtuma mwana wake wa peke katika ulimwengu, ili tupate uzima kwa yeye.(1Yoane 4:9)
19. Kwamaana Mungu alivyopenda ulimwengu hata akamtowa mwana wake wapeke ilikla mtu amwaminiye asipotee, lakini apate uzima wa milele.
20. Kwamaana siionei haya habari njema kwa sababu ni uwezo wa Mungu hata wokovu kwa kila mtu anye amini; kwa muyuda kwanza, na kw muyunani.

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 3:15:Adamu na Hawa wakaasi sheria ya Mungu Wakawa wenye dhambi. Lakini kabla ya kuwatangazia malipizi yao, Mungu akawapa ahadi ya mwokozi atakayemtuma ulimwenguni.

**18. Nitofauti gani kati ya Torati na Injili?**

| Torati | Injili |
|---|---|
| Torati ina tuonyesha nini tunapashwa kufanya.<br>Torati inatuonesha dhambi zetu na hasira ya Mungu. | Injili inatueleza aliyoifanya na anayo endelea kufanya Mungu kwa wokovu wetu.<br>Injili inatufunulia mwokozi wetu na neema ya Mungu. |
| Torati inatushurutisha tumtii kwa ukamilifu. Inatukemea kwa hukumu ya Mungu na ina tuhukumu kwa kifo cha milele. | Injili inatuahidia msamaha wa dhambi zetu, wokovu na uzima wa milele. Inatutolea zawadi hiyo na kutuhakikishia milele. |
| Torati inapashwa kuhubiriwa kwa wote na kwa upekee kwa waovu, wasiojuta na ku tubu, yaani kwa watu wasio tambua dhambi zao na wasio tafuta msamaha. | Injili inapashwa kuhubiriwa , kwa wakosefu wanaotubu, yaani kwa wale wanao tambua dhambi zao na kuomba msamaha |

4. Tunayasema, si kwa hotuba ifundishwayo na hekima ya wanadamu, bali na ile ifundishayo roho, kwa kueleza ukweli wa kiroho kwa watu wakiroho (1Wakorinto 2: 13).

**1. Maneno yote ya Biblia inatoka kwa nani?**

Maneno yote ya Biblia ni ya Mungu. Ni kwasababu hiyo tunasema hamna kosa lolote ndani ya Biblia .Kila kintu kinaposemwa ndani ya Biblia kimevuviwa na kimetoka kwa Mungu.

5. Uwatakase kwa kweli; neno lako ni kweli. (Yoane 17: 17)
6. Kila andiko limevuviwa na Mungu, na linafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki (2 Timoteo 3:16)
7. Maandiko hayawezi kuvunjika (Yoane 10: 35)

**2. Kwanini Mungu ametupa Biblia?**

Mungu ametupata Biblia ili tuokolewe kwa njia ya imani ndani ya Yesu Kristo.

8. Tangu utoto wako umejua maandiko matakatifu; yanaweza kukupa hekima, ili upate wokovu kwa imani ndani ya Kristo Yesu. Kila andiko limevuviwa na Mungu, na linafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki ili mtu wa Mungu awe mukamilifu, ametengenezwa kabisa kwa kuwa tendo njema. (2 Timoteo 3: 17)
9. Neno lako ni taa kwa miguu yangu, na nuru kwa njia yangu.(Zaburi 119: 105)

**3. Twaweza je kutumia Biblia?**

Tunapashwa kulisoma na kujifunza kwa heshima .Kwa hiyo,Tunaweza kusikiya pia yale anayotufundisha. Mwishowe, tuweke tumaini letu kwa yale anayosema na kuishi kufatana na mafundisho.

10. Munatafuta katika maandiko, kwa sababu munazania ya kuwa ndani yao munauzima wa milele; na maandiko haya ndiyo yanayonishuhudia (Yoane 5: 39)
11. Lakini yeye alisema: Afazali heri wale wenye kusikia Neno la Mungu na kulishika.(Luka 11: 28)
12. Lakini Maria akashika maneno haya yote, akayafikiri kwa moyo wake. (Luka 2:19)

## KIBAO CHA KWANZA CHA TORATI

**AMRI YA KWANZA**
**MUNGU**

**« Usiwe na miungu mingine ila mimi tu. »**
**Maana yake nini ?**

Imetupasa kumwongopa, kumpenda na kumtegemea Mungu kuliko vitu vyote.

**24. Wajuaje kwamba Mungu yupo ?**

1. Najua ya kwamba Mungu yupo ninapoona ulimwengu alio umba. Dunia hii kubwa na nzuri kihasi ya kwamba haiwezi kuwako ila kwa mkono wa Mungu tu. Tunaita namna hii ya kujua ufahamu wa umbile wa Mungu.

   21. Kila nyumba imejengwa na mutu ; lakini yeyealiyejenga vitu vyote ni Mungu. (Waebrania 3 : 4)
   22. Muchana unasemezana na muchana, usiku unatolea usiku maarifu. (Zaburi 19 : 2)
   23. Kazi zako ni kubwa sana, Ee Bwana ! Mafikili yako ni mafumbo makubwa. Mujinga hajui ; wala mupumbafu hayafahamu (Zaburi 92 : 5- 6)
   24. Kwa sababu maneno ya Mungu yanayojulikana yanaonyeshwa ndani yao ; kwa sababu Mungu amewaonyesha. Kwa sababu maneno yake yasiyoonekana, tangu kuumbwa kwa ulimwengu yanaonekana wazi, yanafahamika kwa kazi zake, hata uwezo wake wa milele na Uungu wake : wasiwe na uzuru (Waroma 1 : 19 – 20)

2. Ninafahamu kwamba Mungu yupo maana sheria imeandikwa myoyoni mwetu. Tunayaita kama ufahamu wa umbile wa torati Ni Mungu aliye andika ndani ya mioyo yetu.humo. Inatuonyesha kwamba yupo. Angalia swali 16.

## KIBAO CHA KWANZA CHA TORATI

AMRI YA KWANZA
MUNGU

« Usiwe na miungu mingine ila mimi tu. »
Maana yake nini ?

Imetupasa kumwogopa, kumpenda na kumtegemea Mungu kuliko vitu vyote.

**24. Wajuaje kwamba Mungu yupo ?**

3. Najua ya kwamba Mungu yupo ninapoona ulimwengu alio umba. Dunia hii kubwa na nzuri kihasi ya kwamba haiwezi kuwako ila kwa mkono wa Mungu tu. Tunaita namna hii ya kujua ufahamu wa umbile wa Mungu.

25. Kila nyumba imejengwa na mutu ; lakini yeyealiyejenga vitu vyote ni Mungu. (Waebrania 3 : 4)
26. Muchana unasemezana na muchana, usiku unatolea usiku maarifu. (Zaburi 19 : 2)
27. Kazi zako ni kubwa sana, Ee Bwana ! Mafikili yako ni mafumbo makubwa. Mujinga hajui ; wala mupumbafu hayafahamu (Zaburi 92 : 5- 6)
28. Kwa sababu maneno ya Mungu yanayojulikana yanaonyeshwa ndani yao ; kwa sababu Mungu amewaonyesha. Kwa sababu maneno yake yasiyoonekana, tangu kuumbwa kwa ulimwengu yanaonekana wazi, yanafahamika kwa kazi zake, hata uwezo wake wa milele na Uungu wake : wasiwe na uzuru (Waroma 1 : 19 – 20)

4. Ninafahamu kwamba Mungu yupo maana sheria imeandikwa myoyoni mwetu. Tunayaita kama ufahamu wa umbile wa torati Ni Mungu aliye andika ndani ya mioyo yetu.humo. Inatuonyesha kwamba yupo. Angalia swali 16.

29. Hawa wanaoonyesha kazi ya sheria iliyoandikwa katika mioyo yao, zamiri yao ikiwashuhudia vilevile, na mawazo yao yakishitakiana ao kuachiliana (Waroma 2 : 15)

5. Ninafahamu kwamba Mungu yupo maana anajitambulisha ndani ya Biblia. Inaitwa ufunuo au elimu kupita kawaida ya Mungu. Andiko takatifu inahakikisha kwa hiyo kwamba Mungu yupo na inatuzungumzia juu yake.

30. Mimi ni Bwana, ndilo jina langu ; na utukufu wangu sita mpa mwingine, wala sanamu ya kuchonga sifa zangu (Isaya 42 : 8)
31. Lakini Bwana ndiye Mungu wa kweli ; ndiye Mungu aliye hai, mfalme wa milele ; kwa hasira yake inchi inatetemeka, na mataifa hawawezi kuvumilia hasira yake (Yeremia 10: 10)
32. Na huu ni uzima wa milele, wakujue wewe, Mungu pekee wakweli, na Yesu Kristo, uliyemtuma (Yoane 17 : 3)

**25. Nini Biblia yanatufunulia kuhusu Mungu ?**

Biblia inatuonesha Uungu", maana yake aina ya Mungu. Inatuonesha namna eko na namna anatenda.

1) Mungu ni roho. Hana na mwili. Hawezi kuonekana au kuguswa.

33. Mungu ni Roho ; nao wenye kumwabudu sharti wamwabudu katika roho na kweli (Yoane 4 :24)

2) Mungu ni wa milele. Hana mwanzo wala mwisho na habadilike kamwe.

34. Bwana, wewe umekuwa makao yetu, kizazi kwa kizazi. Mbele ya kuzaliwa kwa milima na mbele ya kuumbwa kwa dunia na ulimwengu., milele na milele uko Mungu (Zaburi 90 : 1- 2).
35. Ni mimi wa milele, na sigeuki (Malaki 3 : 6)
36. Wewe, aubaridike, na myaka yako haina mwisho.(Zaburi 102 : 28)

3) Mungu ni muweza yote. Anaweza mambo yote.

37. Wakati Abramu alipokuwa na miaka makumi tisa, Bwana akaonekana kwa Abramu akamwambia : Mimi ni Mwenyezi Mungu ; endelea mbele yangu na uwe mukamilifu. (Mwanzo 17 : 1)
38. Kwani hapana neno lisilowezekana kwa Mungu. (Luka 1 : 37)
39. Yesu akiwatazama akawaambia : kwa watu haiwezekani, lakini kwa Mungu maneno yote yanawezekana. (Matayo 19 : 26)

4) Mungu ni mwenye enzi . maana yake anajuwa yote.

40. Ee, Bwana !Umenitafuta na kunijua. unajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu, unafahamu wazo langu toka mbali unatafuta njia yangu na kulala kwangu, na unajuwa njia zangu zote. Hakuna neno ulimini mwangu usililolijua kabisa, Ee Bwana. (Zaburi 139: 3 – 4)
41. Simoni, mwana wa Yona, unanipenda ? Petro akahuzunika kwa sababu alimwambia mara ya tatu, Unanipenda ? Akamwambia : Bwana, wewe unajua yote ; unajua ya kama ninakupenda. Yesu akamwambia : Kulisha kondoo zangu (Yoane 21: 17)

5) Mungu ni aliyepopote, maana yake yuko pahali pote wakati wote.

42. Mutu ye yote anaweza kujificha pahali pa siri, nisimwone ? Anasema Bwana. Si mimi ninayejaza mbingu na inchi ? anasema Bwana.(Yeremia 23 : 24)

6) Mungu ni Mtakatifu. Hawezi kutenda dhambi. Anatenda mema tu.

43. Mutakuwa watakatifu kwa sababu mimi Bwana Mungu wenu ni mutakatifu. (Walawi 19: 2)
44. Mutakatifu, mutakatifu, mutakatifu ni Bwana wa majeshi : dunia nzima imejaa utukufu wake.(Isaya 6: 3)

7) Mungu ni Mwenye haki. Anapenda mema na kuchukia mabaya.

41. Yeye ni Mwamba, kazi yake ni kamilifu, maana njia zake zote ni hukumu. Mungu mwaminifu asiye na uovu, yeye ndiye mwenye haki na adili. (Kumbukumbu 32 : 4)

8) Mungu ni mwaminifu. Anachunga ahadi zake daima.

42. Kama sisi hatuamini, yeye ankaa mwaminifu ; maana hawezi kujikana mwenyewe.(2 Timoteo 2 : 13)
43. Kwa sababu neno la Bwana ni haki ; na kazi yake yote imetendwa kwa uaminifu. (Zaburi 33 : 4)

9) Mungu ni Mwema. Hawezi kumtendea mutu awayeyote ubaya.

44. Bwana ni mwema kwa watu wote ; na rehema zake ni juu ya kazi zake zote. (Zaburi 145 : 9)

10) Mungu ni Mwingi wa rehema. Hataki kutuapiza kwaajili ya dhambi zetu, bali anatu hurumia.

45. Bwana akapita mbele ya Musa, akatangaza : Bwana, Bwana, Mungu
anayejaa rehema na mwenye neema, si mwepesi kwa hasira, mwenye rehema na kweli nyingi akiwa na rehema kwa elfu za watu, akisamehe uovu na makosa na dhambi ; wala si mwenye kuhesabia mwovu kuwa kama hana dhambi, mwenye kupatiliza watoto uovu wa baba zao, na watoto wa watoto, hata kizazi cha tatu cha na cha ine.(Kutoka 34 : 6 –7)

11) Mungu anajaa faadhili. Anatupenda kwa upenda wa kweli, ingawaje dhambi zetu, anataka kuturehemu.

46. Yeye asiyependa, hakujua Mungu, kwa maana Mungu ni mapendo (1 Yoane 4: 8)

**26. Mungu wa kweli pekee ni nani ?**
Mungu wa kweli pekee ni utatu takatifu. Ni Mungu moja, lakini katika utatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

47. Sikia, Ee Israeli : Bwana Mungu wetu ni Bwana mumoja (Kumbukumbu 6 : 4)
48. Basi, juu ya kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, tunajua ya kuwa sanamu si kitu katika dunia, na ya kuwa hakuna Mungu ila mumoja tu (1 Wakorinto 8 : 4)
49. Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi ( Matayo 28 : 19)
50. Watakatifu wote wanawasalimu ninyi. Neema ya Yesu Kristo, na mapendo ya Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae pamoja nanyi wote.(2 Wakorinto 13 : 13-14).
51. Mimi na Baba yangu ni mumoja. ( Yoane 10 : 30)

## HISTORIA TAKATIFU

Matayo 3 : 16- 17 : Watatu wa utatu takatifu wanajifunua wakati wa ubatizo wa Yesu. Yesu ni Mwana ; Baba husema juu ya mbingu, Roho Mtakatifu hushuka juu ya Mwana kama hua au njiwa.

Mwanzo 1: 26 : Mungu anasema kwa uwingi kwa hiyo, yuko katika utatu, lakini ni mmoja.

**27. Kuna watatu katika utatu takatifu.**
**Tofauti yao ni gani ?**

Siyo rai kujibu swali hiyo. Biblia pekee inatujulisha kuhusu hiyo, na tunakubali mafundisho yake kwa imani.

Kulingana na Biblia, tangu milele yote Baba amemjaa Mwana. Ni mwanzilishi wa Mwana. Ni Mungu kamili, pia siye wala Mwana wala Roho Mtakatifu.

Mwana amezaliwa na Baba. Naye ni Mungu kamili wala siye Baba wala Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu imekuja tangu milele ametoka kwa Baba na kwa Mwana. Naye pia ni Mungu, wala siye Baba wala Mwana.

52. Nitahubiri amri ; Bwana aliniambia : Wewe ni mwana wangu ; leo nimekuzaa. (Zaburi 2 : 7)

53. Lakini wakati Musaidizi anapokuja, nitakayemutuma toka Baba. Roho ya kweli, anayetoka kwa Baba, atanishuhudia (Yoane 15 : 26)
54. Lakini kwa sababu ninyi ni wana, Mungu alituma Roho ya Mwana wake katika mioyo yetu, anayelia : Aba, Baba. (Wagalatia 4 : 6)

**28. Mungu ametukataza nini katika Amri ya kwanza ?**

Mungu ametukataza kuwa na miungu mingine ila yeye. Aabuduye miungu mingine anabudu sanamu.

55. Ndipo Yesu alimwambia : Kwenda zako, Shetani ; kwa sababu imeandikwa, Uabudu Bwana Mungu wako, umutumikie yeye peke yake. ( Matayo 4 : 10)
56. Mimi ni Bwana , ndilo jina langu ; na utukufu wangu sitamupa mwingine, wala sanamu ya kuchonga sifa zangu. ( Isaya 42 : 8)

**29. Je, kuna hakika miungu mingine ?**

La hakuna miungu mingine. Inayoitwa na wapagani, miungu ni masanamu, miungu ya uongo au roho chafu. Angalia swali 111.

57. Basi ninasema nini ? Kitu kilichotolewa sadaka kwa sanamu ni kitu, ao kwamba sanamu ni kitu ? Sivyo, lakini vitu Mataifa wanavyotoa, wanavitolea mashetani, wala si kwa Mungu : nami sipendi ninyi kushirikiana pamoja namashetani. (1Wakorint10 : 19 –20)
58. Wakamutia wivu kwa miungu mingine, kwa machukizo wakamukasirisha. Wakatolea pepo zabihu, si Mungu. Miungu wasiyoijua, miungu mipya iliyotokea siku hizi, Baba zenu wasiyoiogopa. (Kumbukumbu 32 : 16 – 17)
59. Hawakuharibu watu, kama Bwana alivyowaagiza; lakini walijichanganya na mataifa, wakajifundisha kazi zao; wakatumikia sanamu zao; zilizokuwa mutego kwao; ndiyo, wakatoa wana wao na binti zao kuwa zabihu kwa pepo wachafu (Zaburi 106 : 34 –37)

**30. Ni wakati gani unaabudu miungu mingine ?**

1) Nkiweka tumaini katika kitu kinginecho, unaabudu miungu mingine (roho, mtu, irizi au wazo) pahali pakumtumainia muumba pekee. Na aliye mkuu, kiumbe au muumba ? Mungu anatukataza kuabudu vitu alivyo viumba.

49. Lakini Mungu wetu ni mbinguni ; amefanya neno lo lote alilotaka. Sanamu zao ni feza na zahabu, kazi ya mikono ya watu. Zina vinywa, lakini havisemi, Zina macho, lakini hazioni. (Zaburi 115 : 3 – 5)

2) Ukiabudu Mungu asiye utatu takatifu unaabudu miungu mingine.

50. Maana Baba anapenda hamuhukumu, hatamutu mumoja, lakini amemupa Mwana hukumu yote; ili watu wote waheshimu Mwana kama wanavyoheshimu Baba. Mutu yule asiyeheshimu Mwana haheshimu Baba aliyemutuma. (Yoane 5 : 22 – 23)

3) Unabudu miungu mingine kama unaogopa au pepo, mtu, sanamu au mawazo mbaya kuliko Mungu, na kutumainia saana.

51. Musiwaogope wale wanaoua mwili lakini hawawezi kuua nafsi ; lakini zaidi muogope yeye anayeweza kuharibu nafsi na mwili vilevile katika Gehena.(Matayo 10 : 28)
52. Yeye anayependa baba ao mama kupita mimi hanistahili, naye anayependa mwana ao binti kupita mimi hanistahili.(Matayo 10 : 37)
53. Tumainia Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe (Mezali 3 : 5)
54. Maana munajua kabisa, ya kwamba mwasherati wala mtu mchafu wala mweye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, ana uriti katika ufalme wa kristo na Mungu. (Waefeso 5 : 5)
55. Yesu akatazama pande zote, akawambia wanafunzi wake : Kwa matata gani mwenye mali ataingia katika ufalme wa Mungu. ( Marko 10 : 23)
56. Mwisho wao ni uharibifu, Mungu wao ni tumbo, utukufu wao ni haya yao, wananaofikili maneno ya dunia. (Wafilipi 3 : 19)

45. Mupumbafu amesema moyoni mwake : Hakuna Mungu, wao ni wapotevu, wamefanya machukizo ; hakuna mumoja anayetenda mema.(Zaburi 14 : 1)

## HISTORIA TAKATIFU

Luka 16 : 19 – 31 : Yesu anaeleza habari ya mtu moja aliye weka tumaini katika mali yake pahali pa Mungu.

Matayo 19 : 16 –30 : Ni habari ya kijana moja tajiri aliye taka kulinda utajiri wake pahali pakufwata Yesu.

**31. Mungu anatu amuru nini katika amri ya kwanza ?**

Tunapashwa kumwogopa na tukimpenda Mungu na kuweka tumaini yetu yote kwake.

**32. Wakati gani tunaogopa Mungu kuliko vyote?**

Tunamwogopa Mungu kuliko vitu vyote kwa kumheshimu kabisa na kumutukuza kwa moyo wetu wote, kama Bwana wa mbingu na dunia. Tuna muongopa Mungu pia wakati tunapo jitenga na kila kisicho mpendeza.

46. Inchi yote iogope Bwan ; mwenyeji wote wa dunia wamwongope. (Zaburi 33 : 8)
47. Wakati Ambramu alipokuwa na miaka makumi tisa na tisa, Bwana akaonekana kwa Abramu akamwambia : Mimi ni Mwenyezi Mungu ; endelea mbele yangu na uwe mukamilifu. (Mwanzo 17 : 1)
48. Hakuna mutu aliye mukubwa kuliko nimi nyumbani hii, wala hakunikataza kitu ila wewe, kwa sababu wewe ni muke wake ; basi nitafanya uovu mukubwa huu namna gani, na kukosea Mungu ? (Mwanzo 39 : 9)

Dani ya maandiko haya, Yusufu alijubu wadanganifu wa mke wa Bwana wake. Akakataa kufanya mapenzi ya Mungu.

72. Kuogopa Bwana ni kuchukia uovu : majivuno na kiburi, na njia mbovu, na kinywa cha ukaidi ninakichikia. (Mezali 8 : 13)

## HISTORIA TAKATIFU

Danieli 3 : Watu watatu wanamwogopa
Mungu kuliko mfalme, hata
wanapowaamakia kwa mauti.

**33. Wakati gani tunampenda Mungu kuliko vitu vyote ?**

Tunampenda Mungu kuliko vitu vyote kama tukifungana naye pekee kwa moyo wote. Tunampenda pia wakati tunapo jitoa kumtumikia kwa furaha.

26. Akamwambia : Upende Bwana Munguwako na moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. (Matayo 22 : 37)
27. Nina nani mbinguni ila wewe ? Wala hakuna duniani ninayemutaka kuliko wewe. Mwili wangu na moyo wangu inapunguka : Lakini Mungu ni nguvu ya moyo wangu na sehemu yangu milele. (Zaburi 73 : 25 – 26

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 22 : Habari hii inatuonyesha kama
Abramu alimpenda Mungu kuliko mwana
wake.

**34. Wakati gani tunamtumainia saana Mungu ?**

Tunawekea tumaini kwa Mungu wetu kwa moyo wetu wote tunapo toa maisha yetu ndani ya mikono yake.Anatuomba tuifanye kwa siku nzuri na mbaya, katika heri na mateso.

28. Ni heri kukimbilia Bwana kuliko kuamini wakubwa. (Zaburi 118 : 8)
29. Tumainia Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe.(Mezali 3 : 5)

## HISTORIA TAKATIFU

I Samueli 17 : Daudi alikuwa natumaini mwa Mungu na hakuogopa kupigana na Goliata aliye jitu.

AMRI YA PILI
JINA LAKE MUNGU
« USITAJE JINA LA MUNGU WAKO BURE »
Maneno hayo ina maana gani ?

: Imetupasa kumwogopa na kumpenda Mungu, na hivyo tusilitukane jina lake. Kutukana jina la Mungu kwa kuapa, kwa kukufuru na kufanya uganga ao kuishi kwa uwongo na unafiki lakini kila wakati tuliite tuliombe, tulitukuze na kulishukuru kwa beshima.

**Kutusi jina la Mungu :** ni kukosa heshima mbele ya Mungu ao kwa jina lake.

**Kiapo :** ni kuonesha hasira wakati unapo taja jina lake Mungu (tu kiapa) ao kuomba kwa kusema uwongo.

**Kukufuru :** ni kusema maneno mabaya ju ya Mungu, kumutusi ao kumutukana.

**Kufanya uganga :** kutumiya nguvu inayopita mafikiri ya mtu na ya dunia na ukiomba jina la Mungu.

**Kuishi katika uongo ao unafiki :** ni kuonesha picha nzuri kwa inje nyuma yake una ficha kutokuamini kwako.

**35. Luther anafafanuwa hii amri na yote ifwatayo akisema : « Inatupasha kumwogopa na kupenda Mungu kwa hiyo usi.... » Ju ya nini hiyo?**

Kwa sababu utii wa kweli wa amri unatokana kwa kuwogopa na upendo wa Mungu. Sababu ya kutii amri, inapasha kumuogopa na kumpenda.

**36. Jina lake Mungu, ina maana gani ?**

1) « Jina la Mungu » ni jina yote ile Mungu anajipatiya ndani ya Biblia. Yeye ana majina Mengi kwa mfano : Mungu, Mwokozi, mwenyenzi yote, Yesu Kristo, Roho Mtakatifu, Yehovah.

Agano lakale iliandikiwa katika lugha ya kihebrania na katika kihebrania Mungu anaitwa kila wakati Yehovah au Yawe.
Hii jina inamana « Yule eko » katika kifaransa wanaitafsiri kama « Milele » ao « Bwana » kwa mifano ingine tutasoma vitabu vifwatayo : Kutoka 3 : 13-15 : Kumbukumbu 28 : 58 ; Isaya 43 : 15 ; 44 : 6 ; 47 : 4 ; Yeremiya 23 : 6; 32 : 18.

77. Mimi ni Bwana, ndilo jina langu ; na utukufu wangu sitamupa mwingine, wala sanamu ya kuchonga sifa zangu (Isaya 42 : 8 )
78. Katika siku zake Yuda ataokolewa na Israeli atakaa salama ; na jina lake atakaloitwa ni hili, Bwana ni haki yetu (Yeremiya 23 : 6).
79. Naye atazaa mwana : nawe utamwita jina lake Yesu, kwa sababu ndiye atakayeokoa watu wake toka dhambi zao (Matayo 1 : 21).

2) « Jina la Mungu » ni zile zote Mungu anatweleza yeye mwenyewe katika Biblia.

80. Mazabahu ya udongo utanifanyia na kutoa sadaka zako za kuteketezwa juu yake, na sadaka zako za salama, kondoo zako na ngombe zako juu yake ; kwa kila pahali nitakapo kumbusha jina langu nitakuja kwako na kukubariki. (Kutoka 20 : 24).

**37. Nini Mungu ana tukataza ndani ya amri hii ?**

Katika amri hii, Mungu anatukataza kutadja jina lake bure, maana yake bila heshima.

81. Usitaje jina la Mungu wako bure ; maana Bwana hatamuhesabu ya kuwa hana kosa mwenye kutaja jina lake bure. (Kutoka 20 : 7).

**38. Inasema nini « Kutaja jina la Mungu wako bure »?**

1) Kutaja jina la Mungu wako bure ni kutumiya jina moja kwa majina ya Mungu ao Neno lake kwa bure, pasipo sababu ao bila mafikiri kwa yale tunayofanya.
Kunawenye kuapa kwa bure kwa tumiya jina la Mungu. Watu wengini wengine wanazowezi la kusema kwa bure kwamba : « Mungu wangu ». Wengine wanatumiya jina la Mungu sababu ya kuonesha hasira zao. Ni kwa mufano, wakati wanaposema : « jina la Mungu ! » Vitu kama hivi ni vyenye kukatazwa kufwatana Amri ya pili.

2) Wanasema_tena jina la Mungu bule wakati wa kufuru, wanasema mubaya ju ya Mungu na wana mutusi. Maana ingine wakati wana mulaani mwenziwe.
Wana tja bule wakati wanaposema maubiri mabaya. Nikutumiya jina lake Mungu kwa wongo. Tazama swali 42. Kwa wakati mwingine wanataja jina la Mungu kwa bure wakati wana fanya akrofiwa ao uchawi. Mwishoni wana tja bule jina la Mungu kila wakati wana litja bila heshima.

**39. Kukufuru na kulaani, inasema nini ?**

Kukufuru, ni kusema maneno mabaya ju ya Mungu, kumuchekeleya yeye ao kutaja bule jina lake bila heshima. Kulaani, nk kukonesha hasira na kazabu yako kwa muntu mwingine ao kwa kintu. Hata ukiombe kwa muchawi mwana ume ao mwana muke kwa kufanya pahali petu. Sisi wenyewe tunahukumiwa kwa zambi zetu ya kweli.

82. « Na utawaambia wana wa Israeli ukisema : Mutu ye yote anayetukana Mungu wake atachukua dhambi yake. » (Walawi 24 : 15).

83. Kwa ulimi tunasifu Mungu Baba yetu ; na kwa huu tunalaani watu waliofanywa kwa mfano wa Mungu. Katika kinywa kile kile zinatoka baraka na laana. Ndugu zangu, haifai mambo haya kuwa hivyo. » (Yakobo 3 : 9-10).

## HISTORIA TAKATIFU

Matayo 27 : 41 – 44 : wakati wali mupopaYesu musalabani, wayuda wali muchekelea.

2 Wafalme 18 : 17-19 ; 28 : Mufalme wa Asuria akatuma musaidizi wake katika kambi sababu ya kufezeresha wana Israeli akiwasemeya mabaya juu ya Mungu.

Matayo 27 : 24-26 : Wa yuda walilazimisha kifo chaYesu, lakini Pilato hakupenda wamuwe. Walimuombeya kwake Mungu laana wakitenda ubaya.

1 Samueli 17 : 12-54 : Jitu Goliata analaini Daudi na taifa lake Mungu ;

Matayo 16 : 69-75 : Petro alimukana Yesu na anajiombeya gazabu toka kwake Mungu kwa yeye mwenyewe..

**40. Kuapa kwa jina lake Mungu, ina maana gani ?**

Kuapa kwa jina la Mungu, nikuomba Mungu ili awe mushuhuda ya maneno yale tunayo nena na ku musihu atupatiye gazabu kama tunasema wongo.
Bwana wetu anatukataza kusema maneno yasipo maana yao.

84. Lakini ninaita Mungu awe mushuhuda juu ya roho yangu, ya kwamba kwa kuwa hurumia ninyi sijakwenda tena Korinto (2 Wakorinto 1 : 23).

**41. Niwakati gani tunayo wajibu na sheria (ruhusa) ya kuapa kwa jina la Mungu ?**

Tunayo sheria na wajibu ya kuapa kwa jina lake Mungu wakati awiko mbele ya wamzi wana tutazimisha tu seme « na aapa kusema kweli, kweli yote na kweli peke yao » wakati mwingine tuna lazimishwa kuapa juu ya mambo mazuri kwa ajili ya ndugu zetu na utukufu wa Mungu.

85. Ogopa Bwana Mungu wako, na kumutumikiya yeye, na kuapa kwa jina lake. (Kumbukumbu 6 : 13).
86. Kila mutu atii wakubwa wenye amri : kwa maana hapana mamlaka ila kwa Mungu : na mamlaka inayokuwa, imewekwa na Mungu (Waroma 13 :1).
87. Kwa maana watu wanaapia mukubwa kuwapita wenyewe ; na kiapo kinakomesha mabishano yote, na kuhakikisha maneno (Waebrania 6 : 16).

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 24 : 1-9 ; Ibrahimu anaomba kwa mutumishi wake apate kuapa.

2 Wakorinto 1 : 23 : Paulo anaapa kwa mema ya waaminifu wa Korinto.

**42. Ni kwa namna gani kwa kuapa tunatukana jina la Mungu ?**

Tuna tukana jina la Mungu wakati tunapo apa kwa kubeula bila sababu, bila kufili yale tunapo fikiri. Wakati mwingine tuna mutusi wakati tunaapa na mafikiri ya kutenda zambi ao kwa kufichika uwongo. Mwishoni tuna tukana jina la Mungu wakati tunapo akikisha kwa kuapa, Kintu kisipo julikana.

88. Tena mumesikia watu wa zamani walivyoombia: Usiape kwa uwongo, lakini mutimizie Bwana viapo vyoko : lakini ninawaambia ninyi : Usiape kabisa ; wala kwa mbingu, kwa maana ni kiti cha ufalme cha Mungu ; wala kwa dunia, kwa maana ni muji wa Mufalme mukubwa. Wala usiape kwa kichwa chako, maneno yenu Yawe, Ndiyo, ndiyo; siyo, siyo, kwa maana neno zaidi ya haya linatoka kwa yule mwovu. (Matayo 5 : 33-37)
89. Musiape uwongo kwa jina langu, na kuchafua jina la Mungu wako ; mimi ni Bwana. (Walawi 19 : 12)

## HISTORIA TAKATIFU

Matayo 26 : 69-75 : Petro anatukana jina la Mungu : Akiapa kwakudanganya

Matendo ya Mitume 23 : 12-15 : Wa yuda wengine wana apa kwa kutokula kabla ya kumuwa Paulo.

Matayo 14 : 1-12 : Herodia anaapa kuleta kintu tshoshote kwa binti wa Herodia, muke wake wa halali.

**43. Njinsi gani tuatukanapo jina lake Mungu kwa kufanya uganga ao uchawi?**

Tunatukana jina la Mungu wakati tunapofanya unganga ao uchawi, wakati tunapo tumiya jina lake bure ao kwa Neno lake sio ya dunia. Ni kwa msaada wa shetani tunafikia kutumia unganga ao kwa kufanya maneno ya gizaTunatukana tena jina la Mungu wakati tunapo enda kwa wenye kufanya unganga na uchawi kwa kuwaomba msaada.

90. Asionekane katikati yako mumoja anayepitisha mwana wake ao yake kati ya moto, anayetumia maaguzi, anayetenda ubashiri, wala muganga, wala muchawi, wala mupendezi, wala mutu anayepandisha pepo, wala muchawi, wala mutu anayesema na wafu. Kwa maana mutu ye yote anayefanya maneno haya ni chukizo kwa Bwana : na kwa sababu ya machukizo haya Bwana Mungu wako anawafukuza mbele yako. (Kumbukumbu 18 : 10-12)

91. Musiendee wenye pepo wala wachawi ; musiwatafute ili muchafuwe nao; mimi ni Bwana Mungu wenu. (Walwi 19 : 31).

## HISTORIA TAKATIFU

1 Samweli 28 : Mufalme Saulo anapenda kutafuta pepo mubaya ya samweli aliye kufa, kwakuomba msaada.

**44. Je Unajimu inakuwa elimu ya siri (maarifa) ?**

Ndiyo kufwatana na unajimu, Nyota zenye kuvutiwa tukiyo katika maïsha yetu yiyo ni uwongo mutupu. Unajimu kama juwa, mwezi na Nyota iliumbwa na Mungu kwa kutupatiya mwanga, kuonesha mshana na usiku, uhakikisha majaliwa N. K. yiyo inatosha majaliwa hauko wenye Kongozwa na mawazo mnajimu ata mara moja, uko mikononi ya Baba Mungu.

Unajimu inakuwa ni shombo ya shetani sababu ya kuharibu imani ya wana wa Mungu.

Unajimu hiyo ni utafuti wasiansa ya ulimwengu na ma kundana usi tshanganyishe kwa kutolewa unajimu.

94. Umechoka kwa wingi wa mashauri yako. Sasa wale wenye kujua elimu ya nyota, nao wanaotazama nyota, wanaotabiri kila kundama kwa mwezi, wasimame na kukuokoa wewe toka maneno haya yatakayokupata. Tazama, watakuwa kama mashina makavu ya majani, moto utawateketeza ; hawatajiakoa na nguvu za ulimi wa moto ; hautakuwa kaa la kuota moto, wala moto wa kukaa karibu nao. Ndivyo yatakavyokuwa mambo haya uliyojitaabisha nayo, waliofanya biashara nawe tangu ujana wako watatangatanga kila mutu upande wake ; hatakuwa mutu wa kukuokoa. (Isaya 47 : 13-15)

95. Mungu akasema : Iwe miangaza kwa nafasi ya mbingu ipate kutenga kati ya muchana na usiku ; nayo iwe kwa alama na kwa nyakati na kwa siku na kwa miaka. Nayo iwe kwa nuru kwa nafasi ya mbingu, iangaze juu ya dunia ; na ilikiwa hivi. Mungu akafanya miangaza miwili mikubwa ; mwangaza mukubwa kutawala muchana na mwangaza mudogo kutawala usiku ; na nyota vilevile. Mungu akaiweka kwa nafasi ya mbingu kuangaza juu ya dunia, na kutawala juu ya muchana na juu ya usiku, na kutenga nuru na giza ; na Mungu aliona ya kama ilikuwa vema (Mwanzo 1 : 14-18).

**45. Inasema je kutukana jina la Mungu kwa wongo na udanganyifu ?**

Kutukana jina la Mungu kwa wongo na udanganyifu, ni kukufundisha desturi mubaya katika neno lake Mungu. Ni ile wa nabii ya uwongo

wanavyiofanya. Wanatukana tena jina la Bwana wakati wanapoficha mawazo mabaya ndani ya moyo ao maisha ya haya chini ya matendo maovu. Ni hii ifanyao wasio haki.

94. Lakini wananiabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya watu. (Matayo 15 :9)
95. Basi kwa sababu hii mimi ni juu ya manabii hawa, anasema Bwana, wanaoiba maneno yangu kila mutu kwa jirani yake. Tazama, mimi ni juu ya monabii, anasema Bwana, wanaotumia ndimi zao na kusema, yeye anasema (Yeremia 23 : 30-31).
96. Neno lo lote ninalowaagiza ninyi, neno hili muliangalie na kulifanya ; usiongeze juu yake wala usilipunguz (Kumbukumbu 12 :32).
97. Watu hawa wananiheshimu na midomo yao ; lakini moyo wao ni mbali nami (Matayo 15 :8).
98. Si kila mutu anayeniambia : Bwana, Bwana, atakaye ingia ufalme wa mbinguni ; lakini yeye anayefanya mapenzi ya baba yangu aliye mbinguni (Matayo 7 : 21).

## HISTORIA TAKATIFU

1 Mufalme 13 : hii historia inatukumbusha kufa kwa nabii wa Mungu kutokana na udaganyifu wa nabii wauwongo.

Matayo 23 : Walimu wa sheria na mafarisayo ni wanafiki.

Matendo 5 : 1-11 : Historia ya Anania na Safira walio mudanganya Mungu.

**46. Mungu anaturuhusu nini katika amri ya pili ?**

Mungu anatuomba tutaje jina lake na heshima. Anataka tumuombe msaada kwa lazima yetu yote. Tunapashwa kumwanbudu pia, kumusifu na kumushukuru kwa yote anayofanya kwetu.

99. Ukaniite siku ya mateso, nitakuokoa, nawe utanitukuza (Zaburi 50 : 15).

100. Ombeni, nanyi mutapewa ; tafuteni, nanyi mutaona, pigeni mulango, nanyi mutafunguliwa (Matayo 7 :7).
101. Bariki Bwana, ee nafsi yangu ; na vyote vilivyo ndani yangu, vibariki jina lake takatifu (Zaburi 103 : 1).
102. Mukishukuru Mungu ndiye Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo (Waefeso 5 : 20).

## HISTORIA TAKATIFU

Luka 17 : 11-19 : Yesu anaponya waukoma kumi, ila mumoja akarudi kumushukuru.

1 Samweli 1 : 2 : Anna, mama yake na Samweli, yeye akuwa na mtoto, lakini alikuwa naomba Mungu kusudi amupatiye mtoto moja. Kisha yake Bwana alimuptatiya mtoto na alimushukuru kwa moyo mwema.

AMRI YA TATU
NENO LAKE MUNGU
« Uikumbuke siku ya mapumziko na witakase »
Ina maana gani ?

Imetupashwa kuogopa na kumupenda Mungu ili tusikufuru neno lake na mahubiri, ila tuwe na eshima takatifu yakumusikiliza na kumufunza na furaha yote.

**47. Katika Agano la kale wana zungumzia zaidi juu ya sabato inapatana na jumamosi. Ilikuwa ni siku ya kupumzika kwa wa yuda, na iliwapasha kupumzika kwa sababu ilikuwa ni sheria ya Mungu. Kulikuwako na masiku ingine ya karamu. Ni je, kufwatana na amri hiyo, wa christo wana lazimishwa kutimiza siku ya sabato na masiku ingine ya garamu katika agano la kale ?**

Apana, wa christo hawa awalzimishwe kushika siku ya sabato hata siku ingine ya sherehe, kwa sababu Mungu alitosha ma sherla hizo katika agano la kale.

103. Kwani Mwana wa watu ni Bwana ya sabato (Matayo 12 : 8).
104. Basi mutu asiwahukumu ninyi katika vyakula ao vinywaji ao kwa sababu ya siku kubwa, ao mwezi mwandamo ao siku ya sabato. Mambo haya ni kivuli cha maneno ya kuja ; lakini mwili ni wa Kristo. (Wakolosayi 2 : 16-17)

**48. Je Mungu alilazimisha wa christo wa siku izi kushika sabato ya siku moja tu ?**

Apana, hakuna siku kanuni ile wa Kristo wanalazimishwa ku ishika na ku itumikiya.

105. Mutu mumoja anahesabu siku moja kupita siku nyingine ; mwingine anaona kila siku kuwa sawasawa. Kila mutu ajue kabisa katika akili zake mwenyewe. Yeye anayeshika siku, anaishika kwa Bwana : na yeye asiyeshika siku, haishiki kwa Bwana. Naye anayekula, anakula kwa Bwana, kwa sababu anashukuru Mungu : naye asiyekula, hakuli kwa Bwana naye anashukuru Mungu. (Waroma 14 : 5- 6)
106. Munashika siku, na miez, na nyakati, na miaka. Ninawaogopa ninyi, isiwe hakose ninajitaabisha kwenu bule. (Wagalatia 4 : 10-11)

**49. Kwanini tunazishika siku ya jumapili na masiku zingine za sherehe ya kanisa, kama Krismas ?**

Tunashika siku ya jumapili na masiku zingine za sherehe ya kikristo kwa kuifanya Ibada ambamo tunakumbuka mema yote Mungu aliotufanyia kwa ajili ya wokovu wetu.

107. Tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine ; lakini tukionyana, zaidi sana munavyoona siku ile inakaribia.(Waebrania 10 : 25)
108. Walikuwa wakidumu katika mafundisho ya mitume, na katika ushirika, na katika kuvunja mukate na kuomba. (Matendo 2 : 42)

## HISTORIA TAKATIFU

1 Wakorinto 16 : 2 : katika mustari huu, wana zungumuzia mambo ya sadaka dani ya Ibada ya jumapili.

**50. Namna gani ina tunapashwa kufafsiriya Amri ya tatu ngisi isemavyo katika mawazo ya agano jipya ?**

Agano jipya inafundisha ya kama hatuwezi tena kushika sabato kwakuacha ma kazi zote na kuabudu ma Ibada zile siku. Lakini ina tufundisha ya kama inapashwa kuogopa na kupenda Mungu ili tusije kukufuru neno lake na mahubiri. Tunapashwa tuwe na heshima juu yake na utakaso wa eshima kumusikiliza na kumufunza na furaha.

**51. Ni wakati gani tunakufuru amri ya tatu ?**

Tunakufuru kueshimu amri ya tatu wakati tunakufuru neno la Mungu na mahubiri

**52. Ni wakati gani tunakufuru mahubiri na neno la Mungu?**

1) Tunakufuru neno la Mungu na mahubiri wakati tunakosa kwenda ku ibada.
2) Tuna kufuru neno la mungu wakati tunakosa kusoma Biblia.
3) Tunakufuru neno la Mungu na mahubiri wakati tunakosa kusikia neno na atushiriki kusacramenta wakati moja tu ao kwa kuto kuieshimu hii ni namna moja wapo ya kukosa heshima kuneno lake Mungu.

109.Yeye aliye wa Mungu, anashikia maneno ya Mungu ; basi ninyi hamusikii, kwa sababu ninyi si wa Mungu. (Yoane 8 : 47)

110.Yeye anayesikia ninyi, anasikia mimi ; naye anayewakataa ninyi anakataa mimi ; naye anayekataa mimi, anamukataa yeye aliyenituma. (Luka 10 : 16)

## HISTORIA TAKATIFU

Luka 7 : 18-25 : Yesu anasema juu ya Yoane mubatisaji na anaonesha ngisi wa farisayo na walilmu wa sheria walikufuru ubatiso ;

I Samwelil 15 : 10-23 : Saulo hakueshimu neno la Mungu ali itupiliya mbali.

Matendo 13 : 42-52 : Wa yuda wengi hawakua na furaha wakati watu wengi wali amini Yesu Christo katika Antiokia.

**53. Katika amri ya tatu Baba Mungu ana tulazimisha nini ?**

1) Katika amri ya tatu, Baba Mungu ana tuonesha tu pokeye Biblia na mahubiri ya injili kama neno lake.

92. Kwa sababu hii sisi tunashukuru Mungu pasipo kuacha, sababu wakati mulipopokea Neno la Mungu mulilosikia kwetu, mulilipokea si kama neno la watu, lakini, kama lilivyo kweli Neno la Mungu, linalotenda kasi vile ndani yenu munaoamini. (Watesalonika 2 : 13)

93. Maana mukono wangu umefanya vitu hivi vyote, na vitu hivi vyote vimekuwa
Bwana anasema lakini nitaangalia mutu huyu : mutu aliye masikini, mwenye roho ya kupondeka, na anayetetemeka kwa ajili ya neno langu. (Isaya 66 : 2)

2) Mungu ana tulazimisha tu sikiye, tufunze na tufikiri neno lake na furaha.

113. Ufanye angalisho kwa muguu wako wakati umeingiya

nyumbani mwa Mungu, na ujongee kwa kusikiliza, kuliko kwa kutowa sadaka ya bila maana, kwani awajuwe mabaya wanapo fanya

114. Bwana, nimependa makao ya yumba yako, pahali utukufu wako unapokaa (Zaburi 26 : 8)
115. Walikuwa wakidumu katika mafundisho ya mitume, na katika ushirika, na katika kuvunja mukate na kuomba. (Matendo 2 : 42)
116. Neno la Kristo likae kwa wingi ndani yenu kwa hekima yote, mukifundishana na kuonyana kwa zaburi na nyimbo na tenzi za roho, mukiimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. (Wakolosayi 3 : 16)
117. Kitabu hiki cha sheria hakitaondoka kinywani mwako, lakini utawaza ndani yake muchana na usiku, uangalie na kufanya yote yaliyoandikwa ndani yake, halafu utafanyiza njia yako kuwa njia ya baraka na maneno utakayoyafanya yatakuwa vizuri. (Yosua 1 : 8)
118. Lakini yeye alisema : Afazali heri wale wenye kusikia Neno la Mungu na kulishika. (Luka 11 : 28)

3) mungu anatulazimisha tushike, nanguvu kwa namna yote, nahubiri na mafundisho ya
neno lake, kati yetu na katika dunia hii ni
misheni ya kanisa.

119. Tiini wenye kuwaongoza ninyi na kuwanyenyekea ; maana wao wanaangalia kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili wapate kufanya hivi kwa furaha, wala si kwa huzuni : maana hii itakuwa kwenu pasipo faida. (Waebrania 13 : 17)
120. Lakini yeye aliyefundishwa katika neno, ashiriki naye aliyefundisha katika maneno yote yaliyo mema. (Wagalatia 6 : 6)
122. Akawaambia : Kwendeni katika dunia pia, mukahubiri Habari Njema kwa kila mutu. (Marko 16 : 15)

## HISTORIA TAKATIFU

Luka 2 : 41 – 52 : Kijana Yesu alikuwa nashiriki katika Ibada.

Luka 10 : 38 – 42 : Maria alikuwa nasikiya neno la Mungu.

Matendo 17 : 10-15 : Wa christo ya Bérée walikuwa na difunza neno la mungu wakati
wote.

Marko 12 : 41-44 : Mujane anashiriki katika Ibada na analeta sadaka yake, ingawa
alikuwa masikini.

Ona tena mapashwa ya waminifu mbele ya walimu wao na washungaji, hapa juu ukurosa 17.

## JIWE YA PILI YA SHERIA

**54. Namna kani tunaweza kufanya muhtasari ya sheria la jiwe ?**
Jibu kwa hiyo swali inapatikana ndani ya maneno ya yesu : "Na ya pili inafanana nayo ni hii : Penda jirani yako kama wewe mwenyewe." (Matayo 22 : 39)

**55. Jirani yetu ni nani ?**
Mtu yeyote ni jirani yetu, saidi wakati ana haya (lazima) na usaidizi wetu.

121. Basi, tukiona nafasi, tutende mema kwa watu wote, zaidi kwao walio wa nyumba ya imani. (Wagalatia 6 : 10)

123. Lakini mimi ninawaambia ninyi :
Pendeni adui zenu, muwabariki wenye uwalaani ninyi, muwatendee mema wenye kuwachukia ninyi, muwaombee wenye kuwazarau, na kuwatesa ninyi.(Matayo 5 : 44)

**56. Namna gani twaweza kupenda jirani yetu ?**

Inatu pasha kupenda jirani yetu kama vile tuna jipenda sisi wenyewe na kuonesha upendo kwa kushika ma amri ya pili ya jiwe la sheria.
Kufwatana nama amri kwanziya 4 mpaka 10 wana tuonesha ngisi inatupasha kufanya mbele ya jirani yetu.

124. «Basi yo yote munayotaka watu wawatendee ninyi, ninyi muwatendee vivyo hivyo ; maana hii ni torati na manabii. » (Matayo 7 : 12)

## HISTORIA TAKATIFU

Luka 10 : 25-37 : Yesu anaeleza katika mfano ju ya kufasiriya namna gani inatupasha kupenda jirani yetu.

> AMRI YA NNE
> WAZIZI NA VYONGOZI WETU
> « Ueshimu baba na mama yako, ili uwe heri na upate kuishi siku ningi duniani »
>
> Ina maana gani ?
> Inatupashwa kumuogopa na kupenda Mungu ili tusi zarau ao ku usikisha wazazi na vyongozi wetu. Inatupasha zaidi kuwa heshimu, ku wasaidiya na kuwatii katika upendo na heshima.

**57. Katika tafsiri ya Amri hiyo, inahusu wazazi na vyongozi wetu. Vyongozi wetu ni nani ?**

Vyongozi wetu ni wale wote, kutosha wazazi wetu, weko na mamlako ju yetu. Wana itwa kufwatana na mupango wa uubaji wa Mungu kwetu ili watuongoze.
Tuna kuwa na vyongozi wa masomo, katika fasi ya kazi na ndani ya serkali.
Tazama horoza kuu ifwatayo : wazee, Mkuu wa kijiji, Mukuu wa Jimbo, mwalimu wa masomo, Mkuu wa chuo, Kamanda, Polici, wa askari, mkuu wa kazi, Raisi wa inchi, na ote wanatuongoza.

125. Jicho la mutu anayezihaki baba yake, na kuzarau kutii mama yake,kunguru za bonde watalingoa na wana-tai watalikula. (Mezali 30 : 17)
126. Hivyo yeye anayeshindana na mwenye mamlaka, anashindana na amri ya Mungu; nao wanaoshindana watajipatia hukumu. (Waroma 13 : 2)

## HISTORIA TAKATIFU

1 Samweli 2 : 12-18 : Watoto wa kuhami Elie hawaku heshimu hata baba yao hata sheria ya Mungu.

2. Samweli 15 : Absalom asikueshimu uuwongozi wa Baba yake David, yeye alikuwa ni Mufalme.

2 Mufalme 2 : 23-25 : Watoto wa nabii Elisée walikosa eshima ikwake na Mungu aka waapiza.
Tazama tena mapashwa yetu mbele ya vyongozi yetu huko juu p. 17-19

## 59. Mungu anatuamuru nini katika amri ya ine ?

1) Mungu anatuamuru tueshimiye wazazi wetu. Inatupasha tu watazeme kama wenyeviti wake apa duniani, kuwapenda na kuwapatiya na fasi kama zawadi yetu ya zamani.

127. Simama mbele ya wenye imvi na heshimu uso wa muzee, na utaogopa Mungu wako ; mimi ni Bwana. (Walawi 19 : 32)
128. Heshimu baba yako na mama yako (hil ni amri ya kwanza yenye ahadi) upate heri, na uishi siku nyingi katika dunia. (Waefeso 6 : 2-3)

2) Mungu anatulazimisha kuwasaidiya wazazi wetu na vyongozi wetu, tukihakikisha kwa furaha mapashwa yetu kwao.

Lakini kama mujane ana watoto ao wajukuu, wajifundishe kwanza kuonyesha heshima kwa nyumba yao wenyewe, na

**70. Ni aina gani ya ndowa Mungu anakubali ?**
Mungu anakubali aina tatu ya ndowa wakati mume na muke wanajulikana na watu katika masingira yao kama wanaowana kihalali.

## HISTORIA TAKAFU

2 Wafalme 19:
2 Wafalme 6: 8-23
Danieli 3 na 6:
Luka 16: 19 –31:

**118. Biblia tweleza nini Kunsu wamalaika wabaya?**
Biblia inatweza ya kama wa malaika wali asi Mungu baada ya kuumbwa kwao mukubwa wao anaitwa Shetani wanakuwa adui ya Mungu na ya watu. Bwana ali watupa kwa milele. Wao hawawezi kuokolewa.
Wa malaika wabaya ni wengi, wenye nguvu na wakali wao ni mapepo mbaya Biblia inayotweleza wa baya ni na roro mubaya naotenda katika madini isiyo amini Yesu. Ina tupasa kujua kama si ma roho ya wa kambo wetu wa zamani inatutakia mabaya, lakini ma roho mabaya, wale wa malaika waliofanya zambi, wale Biblia inaita ma pepo mbaya kyahiyo sisi hatuwezi ku waogopa, sbabu Yesu Kristo anawashinda. Na tuwezi ku wa abudu. Lakini inatupasa kuwa wangalifu na ku wa shinda, kwasababu wana toka ku tajaribu ha kututenda na Mungu.

265. Kwa maana ikiwa Mungu hakuanchilia malaika wakati walokosa, lakini aliwatupa shimoni, na kuwatia katika vifungo vya giza walipokosa, lakini aliwatupa shimoni, na kuwatia katika vifungo vya giza walindwe hata hukumu. (2 Petro 2: 4)
266. Kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama, lakini juu ya falme na mamlaka, juu ya watawala wa ulimwengu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika pahali pa mbingu. (Waefeso 6: 12)
267. Akamwuliza: Jina lako nani? Akamujibu: Legioni (maana: Jeshi), kwa sababu sisi ni wengi (Marko 5: 9)
Nnyi wa baba yenu Shetani na tamaa za baba yenu munataka kuzifanya. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, na hakukaa

katika kweli; kwa sababu hakuna kweli ndani yake. Wakati anaposema uwongo, anasema yaliyo yake mwenyewe, kwa sababu yeye ni muwongo, na baba ya wongo. (Yoane 8: 44)

269. Muwe na kiasi na kuangalia; adui yenu Shetani, kama simba ya kunguruma anazungukzunguka akitafuta mutu amumeze. Nanyi mushindane naye katika imani yenu, mukijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walio duniani (1Petro 5: 8 – 9)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 3: 1 – 7: Shetani anajaribu Adamu na Awa.

Ayubu 1 na 2: Shetani anajaribu kuharibu imani ya Ayubu.

Matayo 4: 1 – 11: Yesu anashinda majaeibu ya Shetani .

## MTU

**119. Kiumbe gani kinapita vuimbe vyobe vinavyo one kuna?**

Mtu ni kiumbe kinapopita viumbe vyote vinayo onekana kwa kuumba dunia, miti na wanyama, Mungu kwasantu alisema, na viumbe vikawa. Lakini kwa kuumba, mtu, akatengeneza mwili kwa ndongo na liska akapiliza Mungu alifanya mtu kuwa kiumbe kwenye elimu ya kipeke. Lakini Mungu aliu umba kwa mfano wake.

270. Bwana Munfu akafanya mutu wa mavumbi ya inchi, akapuliza pumuzi ya uzima ndani ya pua yake; na mutu alikuwa nafsi ya uhai (Mwanzo 2: 7)

271. Mungu akaumba mutu kwa mufano wake mwenyewe, kwa mufano wa Mungu akawumba; mume na muke akawaumba. (Mwanzo 1: 27)

**120. Mtu alikuwa namna gani wakati aliumbwa kuamba dunia, miti na wanyama, Mungu kwasantu alisema, na viumbe vikawa.**

Wakati mtu aliumba kwa "mfano wa Mungu" ali fahamu Bwana. Ufahamu huu ili mutia katika furaha. Alikuwa mwenye haki na mtakifu, mana yake wasio zambi.

2) Mungu anatukataza kufanya mubaya kwa jirani yetu, maana yake kuzuru maisha ao afya yake, kwa matendo yetu na masemo yetu.

137. "Wapenzi, musijilipize kisasi, lakini kukiacha kwa gazabu ; maana imeandikwa : kisasi ni changu, mimi ; mimi nitalipa, Bwana anasema." (Waroma 12 : 19)

3) Mungu anatukataza kuharibu maisha yetu wenyewe hakuna hata mtu mumoja anaye ruhusiwa kudiuwa mwenyewe, kwasababu ni kiumbe chake Mungu. Tena mtu asiye amini akijiuwa hana uwezo yakutubu hata kupata msamaha na uzima wa milele.

4) Mungu anatukataza kulinda hasira ndani ya mioyo yetu, fitina na unafiki kwa jirani yetu.

138. "Lakini mimi ninawaambia ninyi : kila mutu anayekasirikia ndugu yake itamupasa hukumu ; na kama mutu akisema na ndugu yake, Raka, itamupasa baraza ; na mutu akisema, mupumbafu, itamupasa Gehena ya moto. (Matayo 5 : 22)
139. "Kila mutu anayechukia ndugu yake ni mwuaji : nanyi munajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake." (1 Yoane 3 :15)
140. " Kwani kwa moyo yanatoka mawazo mabaya, uuaji, uasherati, uzini, wizi, ushuhuda wa uwongo, matukano." (Matayo 15 : 19)
141. "Mukasirike na musifanye dhambi ; jua lisishuke na uchungu wenu haujakwisha bado." (Waefeso 4 : 26)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 4 : 1-16 : Mungu anaweka Kaina katika angalifu, ila Kaina hakubali shauriyake aka uwa ndugu yake Abel, kwa sababu alimusikiliya wivu kwake.

Kutoka 21 : 28 – 36 na Kumbukumbu 22 : 8 : hiyo ni sheria Mungu alileta kwa taifa ya Israeli ju ya uwadi kwa kukufuru ao kwa kusahau.

Matayo 27 : 3-10 : Baada ya kumtowa Yesu, Yuda alijitiya mwenyewe katika kukata tamaa.
1 Samweli 31 : Saulo alijiuwa kusudi hasiuwawe na adui wake.

1 Mufalme 16 : 15-22 : Zimri alijiuwa kwa kwepukana na adui wake.

Mwanzo 37 : 12-36 : Wandugu wake Yosufu wali tabisha maisha yake kwa Kumuchukiza.

Kutoka 1 : Wamisri wanatesa waebrania kwa kuwatabisha katika maisha mabaya ya nguvu.

Matendo 6 : 8-7 : 60 : Wa Yuda aliuwa Stefano kwa chuki.

**62. Mungu anatuamuru nini katika amri hii ya tano ?**

Katika amri hiyo ya tano, Mungu ana tulazimisha tuwasaidiye jirani yetu. Tuwasaidiye wakati weko katika hatari ao katika maitaji, kuwasikiliya huruma wakati anapoteseka na tuwe na juhudi kwao tukiwa na moyo ya upendo, wa kimya na wa majajiliano.

142. "Kama basi adui yako akiwa na njaa, umulishe ; kama akiwa na kiu, umupe cha kunywa ; maana kwa kufanya hivi, utaweka makaa ya moto juu ya kichwa chake." (Waroma 12 : 20)
143. "Heri wenye upole : maana wao watariti inchi. Heri wenye rehema : maana wao watapata rehema. Heri wenye kufanya salama : maana wao wataitwa wana wa Mungu." (Matayo 5 : 5, 7, 9)
144. "Patana na mushitaki wako upesi, ungali unapokuwa pamoja naye njiani, mushitaki asije, atakupeleka kwa mwamuzi na mwamuzi atakupeleka kwa askari, na utatupwa katika kifungo." (Matayo 5 : 25)
145. "Kwa sababu kama ninyi munasamehe watu makosa yao, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi vilevile. Lakini kama ninyi hamusamehe watu makosa yao, Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu vilevile." (Matayo 6 : 14, 15)

146." Na mwonyeshe mema ninyi kwa ninyi, muwe wenye huruma, mukisameheana, kama Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi." (Waefeso 4 : 32)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 14 : Abraham anaokowa musikuli wake Loti mbele ya wafalme wanafiki.

1 Samweli 26 : Daudi ana sababu ya kuuwa Saulo, ila anakataa, alafu Saulo anataka mpaka amuuwe Daudi.

Luka 10 : 25-27 : Yesu anasemeleya mfano wa Musamaria mwema.
Luka 17 : 11-19 : yesu anatunza waukoma kumi.

Matayo 8 : 5-13 : Yesu anatunza mutumishi wake akida waroma, ila waroma walikuwa ni wanafiki wa wayuda.

Mwanzo 45 : 1-16 ; 50 : 15-26 : Yosefu anasamehe zambi ya wandugu wake.

**AMRI YA SITA**
**UTAKASO NA NDOWA**
« Usi zini »
Ina maana gani hiyo ?

Inatupasa kuogopa na kupenda Mungu ili tuwe safi na wenye kutakasiwa katika mafikili yetu, katika maneno yetu na katika matendo yetu. Inatupasa tena kupendana na kueshimiyana katika ndowa.

### 63. Ndowa ni nini ?

Ndowa ni upatanisho kati ya muume na muke. Iliandaliwa na Mungu. Katika ndowa nmuume na muke wanaunganishwa kwa maisha, kufwatana kanuni ya mila na desturi zao kama vile sheria inashindiliya ndani ya inchi yao. Ushumba unaitwa azizo ya kuunga na

siku moja katika ndowa. Kufwatana na neno la Mungu, muume na muke wana kuwa mwili mumoja, maana yake kintu kimoja.

147.« Akajibu, akasema : hamukusoma ya kama yeye aliyewafanya toka mwanzo aliwafanya mume na muke, na alisema : kwa sababu hii mume ataacha baba yake, na mama yake, na ataambatana na muke wake ; nao wawili watakuwa mwili mumoja. Hata wamekuwa, si wawili tena, lakini mwili mumoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mutu asiwatenganishe.» (Matayo 19 : 4—6)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 2 : 18-24 : Makala hii inaeleza ndisi Mungu peke yake aliandaa ndowa.

Matayo 1 : 18-20 : uchumba wa Mariamu na Yosefu.

**64. Nini Mungu anatukataza katika amri ya sita ?**

1) Katika amri ya sita, Mungu anatukataza kuvunja mapatano ya ndowa.
   a. Kama muume anafanya mapatano ya aibu na muke asiye wake ao kama muke piya anafanya mapatano ya aibu na muume asiye wake, anatenda usharati na wanavunja patano ya ndowa. Iumbali na sheria ya Mungu.
   b. Kama muume anaasha muke wake ao muke anaasha mume wake, wanavuja patano ya ndowa ; ni tena umbali na sheria ya Mungu.

148. «Hata wamekuwa, si wawili tena, lakini mwili mumoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mutu asiwatenganishe. » (Matayo 19 : 6)
149. «Ninawaambia ninyi, kila mutu atakayeondosha muke wake ila kwa sababu ya uasherati, na kuoa mwingine, anazini ; naye anayemwoa yeye aliyeondoshwa anazini. » (Matayo 19 : 9)
150. «Ndoa iheshimiwe na watu wote, na kitanda kisiwe na uchafu : kwa sababu Mungu atahukumu waasherati na wazini. » (Waebrania 13 : 4)

2)Katika amri ya sita, Mungu anatukataza tena inafikili yote, maneno yote na tamaa yote ya uchafu.

131. "Kwani kwa moyo yanatoka mawazo mabaya, uuaji, uasherati, uzini, wizi, ushuhuda wa uwongo, matukano."(Matayo 15 : 19)

132.«Mumesikia watu wa zamani walivyoambiwa : usizini ; lakini mimi ninawaambia ninyi kila mutu anayetazama mwanamuke kwa kumutamani, amkwisha kuzini naye moyoni mwake. » (Matayo 5 : 27, 28)

133.«Lakini uasherati usitajwe katikati yenu, wala uchafu wo wote wala kutamani, kama inavyostahili watakatifu ; wala aibu wala masemo yasiyo na maana, wala maneno ya kuchekesha yasiyofaa ; lakini zaidi maneno ya kushukuru. » (Waefeso 5 : 3, 4)

134.«Wala musishirikiane na matendo ya giza yaiyozaa matunda, lakini zaidi muyahamakie ; kwa maana ni haya kusema juu ya maneno wanayoyafanya kwa siri. » (Waefeso 5 : 11, 12)

## HISTORIA TAKATIFU

2 Samweli 11 : Mafikili mabaya ya Daudi ili musukuma kutenda usharati na uwadi.

Marko 6 : 17-20 : Herode alidingunisha kwa ndowa na muke wa ndugu yake.

Mwanzo 39 : 1-20 : Yosefu anapinga tama mubaya ya muke wa Potiphar, kyongozi wake.

Wamzi 16 : Hali ya Samsoni mbele ya wana wake haikukuwa safi.

## 65. Ninini Mungu anatulazimisha katika amri ya sita ?

135.«Wapenzi, ninawasihi ninyi, kama wageni na wasafiri, mukatae tamaa za mwili zinazopigana na roho. (1 Petro 2 : 11)

«Kwa kumaliza, ndugu zangu maneno yo yote yaliyo ya kweli, maneno yo yote yaliyo ya heshima, maneno yo yote yaliyo haki, maneno yo yote yaliyo safi, maneno yo yote yenye «Kwa kumaliza, ndugu zangu maneno yo yote yaliyo ya kweli, maneno yo yote yaliyo ya heshima, maneno yo yote yaliyo haki, maneno yo yote yaliyo safi, maneno yo yote yenye

kupendeza, maneno yo yote yenye sifa njema ; ukiwa wema wo wote na ikiwa sifa yo yote, fikilieni maneno haya. » (Wafilipi 4 : 8)

157. «Masemo maovu yasitoke vinywani mwenu, lakini yaliyo mema kwa kujenga kama inavyohitajiwa, yawape neema wale wanaosikia. » (Waefeso 4 : 29)

**66. Imetupasa tufanye nini ndani ya amri ya ujinsia ya maisha ya kupendeza Mungu.**

1) Kwakujifunza neno la Mungu, kwakuomba, kwakufanya kazi na kwakutengeneza nia yetu, tunapasa kukombaniza tama yetu na mawazo mubaya yetu.

129. «Hakuna mutu aliye mukubwa kuliko mimi nyumbani hii ; wala hakunikataza kitu ila wewe, kwa sababu wewe ni muke wake ; basi nitafanya uovu mukubwa huu namna gani, na kukosea Mungu ? » (Mwanzo 39 : 9)

130. « Unirudishie furaha ya wokovu wako ; unitegemeze kwa roho ya tayari. » (Zaburi 51 : 12)

131. « Wewe usiangalie mvinyo wakati ilipo nyekundu, wakati inapotoa rangi yake ndani ya kikombe, wakati inaposhuka pasipo matata. Kwa mwisho inauma kama nyoka, na kuchoma kama fira ; macho yako yatatazama mambo mageni, moyo wako utatoa maneno yasiyofaa. » (Mezali 23 : 31-33)

2) Inatupasa kuogopa majaribu yote ya kutupakaa mukoshi na tukio yote inatupeleka katika zambi.

132. «Kimbieni uzini. Kila zambi mutu anayofanya ni inje ya mwili ; lakini yeye anayefanya uzini anafanya zambi juu ya mwili wake mwenyewe. Hamujui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mutakatifu alilye ndaniyenu, muliyepewa na Mungu ? Na ninyi si mali yenu wenyewe ; kwa sababu mulinunuliwa kwa bei ; basi tukuzeni Mungu katika mwili wenu na katika roho yenu, maana ni ya Mungu. » (1Wakorinto 6 : 18-20)

162.«Usihamakie muzee, lakini umwonye kama baba ; na vijana kama ndugu ; wanwake wazee kama mama ; wanawake vijana kama ndugu, kwa usafi wote. » (1Timoteo 5 : 1, 2)

163.«Lakini kimbia tamaa za ujana ; ukafuate haki, na imani, na mapendo na salama, pamoja nao wanaoita Bwana kwa moyo safi. » (2 Timoteo 2 : 22)

164.« Mwana wangu, kama wenye zambi wakikushawishi, usikubali. » (Mezali 1 : 10)

165.«Na ilikuwa kwa wakati huu, akaingia nyumbani kufanya kazi yake ; wala hakuna mutu wa watu wa nyumba aliyekuwa nyumbani. Akamushika kwa nguo yake, akasema : Lala nami ; akaacha nguo yake mukononi mwake, akakimbia, akatoka inje. » (Mwanzo 39 : 11, 12)

**67. Ni mapashwa gani iliyo yapeke kwa wenye ushi katika ndowa ?**

Wenye kuishi katika ndowa wanapashwa kupendana, kweshimiyana na kusaidiyana moja kwa mwingine. Muume anapashwa kutazama muke wake kama musaidizi wake Mungu alimupatiya na kumupenda. Muke anapashwa kutazama muume wake kama musaidizi wake Mungu alimupatiya, amupende na kumutii. Tazama kanuni ya nyumba, ha ju NK 18.

166.« Lakini kama vile kanisa linvyotii Kristo, hivi vilevile wake watii waume wao katika kila kitu. Waume, mupende wake wenu, kama vile Kristo alivyopenda kanisa, na kujitoa mwenyewe kwa ajili yake.

**68. Tunaweza kusema nini kuhusu mitala (polygamie) ?**

Biblia inatufundisha ya kama watu wengi katika Agano la kale walikkuwa naishi katika mitala kama vile alikuwa, kwa mfano, Abrahamu, yakobo na Daudi. Abraham akashukuwa Agai kama muke wa pili. Mungu hakuitikiye mtoto wa Agar kama muriti wa agiso yake, ila hakusema neno yoyote kuhusu mitala ya kuhani. Daudi alisini na Batiseba, muke wa uri Mungu alimuapiza kwa sababu ya hayo ila hakumulaumu kuhusu mitala kwahiyo, ndowa kama vile iliandaliwa kwa ku umbwa ulilmwengu ilikuwa ni ndowa ya muke mumoja tu, ungano ya muume na muke.

582.Tazameni, ni mapendo namna gani tuliyopewa na Baba, tuitwe wana wa Mungu. Kwa sababu hii dunia haitutambui, kwa sababu haikumutambua yeye.(1 Yoane 3 : 1)

583.Kwa maana hamukupokea tena roho ya utumwa inayoleta woga, lakini mulipokea roho ya kufanywa wana, kwa sababu hii tunalia ; Aba, Baba. (Waroma 8 : 15)

**227. Sababu gani tunasema "Baba yetu" ?**

Tunasema "Baba Yetu" sababu kila mwamini ni mtoto wa baba moja. Juu ya wema Yesu Kristo alifanya juu yao. Nanaomba sisi wote pamoja hawa kwawale na hawa kwa wengine.

584.Mungu mumoja, naye ni Baba ya wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.(Waefeso 4 : 6)

585.Maana ninyi wote ni wana wa Mungu, kwa imani, katika Yesu Kristo. (Wagalatia 3 : 26)

**228. Sababu gani tunaongeza kama "Aliye mbinguni"**

Neno "Aliye Mbinguni" inatukumbusha kama Mungu ni Baba yetu, na ni bwana. Mwenyi nguvu. Anaweza kufanya zaidi ya mipaka kupita yale tunaomba ao tukiwaza.

586.Basi kwake yeye anayeweza kufanya mambo kuliko yote tunayoomba ao kufikili, kwa kadiri ya uwezo unaotenda kazi ndani yetu, kwake uwe utukufu katika kanisa na katika Kristo yesu hata vizazi vyote kwa milele na milele. Amina. (Waefeso 3: 20, 21)

**229. Kuna kuwa nini kati ya maulizo saba iliyo ya maombi ya Bava yetu ?**

Ndani ya maombi tatu ya kwaanza, inakuwa ni ulizo juu ya Baraka ya kiroho. Mu ya ine, tunaomba juu ya maisha ya mwili wetu, na ndani ya hiyo tatu ya mwisho, tunaomba kwa Mungu atuokowe kwa mabaya.

| Maombi n° 1-3<br>Jina lako lisifiwe<br>Ufalme wako uje<br>Mapenzi yako ya fanike hapa duniani kama mbinguni. | Ombi n° 4<br>Utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku | Maombi n° 5 – 7<br>Utusamehe deni zetu kama sisi vile vile tunavyosamehe wadeni wetu.<br>Usitulete katika majaribu lakini utuokoe na yule mwovu |
|---|---|---|
| ↓ | ↓ | ↓ |
| ↑ | ↑ | ↑ |
| **(Mabaraka ya roho)** | **(Kwa maisha ya mwili)** | **(Kutuokowa ku majaribu)** |

**OMBI YA KWANZA**
"Jina lako litukuzwe"
Ina maana gani ?

Jina la Mungu nitakatifu kwa yeye peke, lakini ndani ya ombi hiyo tunaomba kama asifiwe katikati yetu.

Inatugfaa nini juu ya jina lake Mungu iwe yenyi kutukuzwa kwetu ?

Inafai neno la Mungu lifundishwe kwa ukweli, katika utakaso, juu tukaishi kwa utakaso sawa watoto wa Mungu. Juu Baba wetu wa Mbingu apate kutukubali wema huu ! Lakini yeyote anayefundisha ao kuishi na muna isiofaa anakufuru kati yetu jina la Mungu. Na baba wetu wa mbingu anatukinga kwa hiyo.

**230. Nini inafaidia ndani ya ombi hii ya kwanza?**

Ndani ya ombi hii ya kwanza, tunaomba juu na jina la Mungu isifiwe na ieshimiwe namuna inayo pasayo katikati yetu.

**231. Ni je jina la Mungu linasifiwa na kweshimiwa na muna inayo faa kati kati yetu ?**

1) Jina la mungu linasifiwa na kweshimiwa wakati neno lake linafundishiwa kwa ukweli na kwa uhaki.

    587.Uwatakase kwa kweli ; neno lako ni kweli.(Yoane 17 : 17)
    588.Nabii aliye na ndoto, aseme ndoto yake ; na yeye aliye na neno langu, kwa uaminifu. Majani makavu ni kitu gani kuliko ngano ? anasema Bwana. (Yeremia 23 : 28)

2) Jina la Mungu linasifiwa na kweshimiwa w<akati sisi tuitwa watoto wake, tunaishi maisha ya utakaso, kufuatana na neno lake Mungu;

    589.Vivyo hivyo nuru yenu iangaze mbele ya watu, waone matendo yenu mazuri, watukuze Baba yenu aliye mbinguni. (Matayo 5 : 16)

**232. Tunakufuru je jina la Mungu ?**

1) Jina la Mungu linakufuria wakati wanafundisha ma elimu iendayo kingume na neno lake.

    590.Makuhani yake wamefanyia sheria yangu kwa jeuri na wamechafua vitu vyangu vitakatifu ; hawakuweka tofauti ya vitu vitakatifu na ya siku zote ; wala hawakufundisha watu kutambua vitu vichafu na vitu vilivyo safi, na wamefichia sabato zangu macho yao, na nimetiwa uchafu katikati yao. (Ezekieli 22 : 26)

2) Jina la mungu linakufuria wakati tunapoishi namuna isiyo faa na neno lake.

    591.Wewe mwenye kujisifu katika sheria; kwa kuvunja sheria unazarau Mungu ? Kwa maana jina la Mungu linatukanwa katikati ya mataifa kwa sababu yenu, kama ilivyoandikwa. (Waroma 2 : 23, 24)

**OMBI LA PILI**

"Ufalme wako ujo"

Ina maana gani ?

Utawalo wa Mungu inajiweka nayeye peke ulimwengu nzima, na haina lazima, juu ya hiyo na maombi yetu, lakini tunaomba tu kama uje tena kwetu (ijitukuzwe).

Je utawalo wake Mungu inakaa kwetu ?

Utawalo wake Mungu inakaa kwetu wakati anapotugabiza Roho wake Mtakatifu, juu sisitufikie kwamini wema wake kupitia sauti yake na kuishi kwa utakaso, tangu sasa hata milele.

**233. Ni kwa utawalo gani ilio ndani ya ombi ya pili?**

Hii ulizo inayokuwa ndani ya ombi ya pili, si juu tu ya utawalo ya uwezo wake Mungu, lakini kwa utawalo wa nema, hii utawalo ni hiyo anatumia ndani ya enjili wakati anapo auzisha kukamilisha, kwa kuwa kanisa lake hapa ulimwengu anayo sindikiza kwa maisha ya milele. Ikiwa kwa wale wamini wanao kuwa mbinguni, weko zamani ndani ya utawalo wa sifa yake.

**234. Inakuwa na nia kani hii ombi ?**

1) Tunaomba kwa Mungu atukubalie neema ya imani ya kweli na maisha ya kupendeza kwa neno lake.

592.Akisema : wakati umetimia, ufalme wa Mungu ni karibu. Tubuni mukaamini Habari Njema. (Marko 1: 15)
593.Basi kama mulivyopokea Kristo Yesu Bwana, mutembee vivyo hivyo ndani yake. (Wakolosayi 2 : 6)

2)Tuna muomba tena utawalo wake wa neema ipate kwenea ulimwengu wote.

594.Ombeni basi Bwana ya mavuno atume watenda kazi katika mavuno yake. (Matayo 9 : 38)
595.Kwa mwisho, ndugu, mutuombee, hata neno la Bwana liendelee na kutukuzwa, kama inavyokuwa kwenu. (2 Watesalonika 3 : 1)

Tunaomba pia hajarikishe kuja kwa utawalo wa sifa lake.

596.Musiogope, kundi dogo, kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ninyi ufalme. (Luka 12 : 32)
597.Yeye anayeshuhudia maneno haya anasema : ndiyo ; ninakuja upesi. Amina, kuja Bwana Yesu. (Ufunuo 22 : 20)

**HISTORIA TAKATIFU**

Matendo 4 : 23-31 : Mwaminifu wameombea Neno la Mungu lisambaswe duniani mzima.

**OMBI YA TATU**

"Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni"

Ina maana gani ?

Mapenzi ya Mungu ni mema na ya rehema, ya natimizwa ulimwengu ni pote na hana lazima, hayo yote kwa maombi yetu. Natunaomba ya timizwe tena katikati yetu.

Je mapenzi ya Mungu yanatimizwa kati yetu ?

Mapenzi ya mungu yanaitmizwa wakati Mungu anasimanmisha na kuvunja mabaya ya mipango na yote mawazo mabaya inayotuzuiza katika utakaso wa jina lake na kupinga ata kuja kwa utawalo wake. Mapenzi yake yanatimizwa tena wakati ana tusubutisha na kutushika kabisa ndani ya neno lake na katika imani ya kweli ata mwisho wa maisha yetu. Hiyo ndjo wema na rehema ya kushinda.

**235. Ni uzuru na rehema gani ya Mungu kupita ? Na anataka nini ?**

Mungu anataka jina lake lisifiwe na kueshimiwa ata ulimwengu nzima inamishwe ndani ya utawalo wake.

**236. Tunaufahamu gani juu ya mapenzi ya Mungu ?**

1) Mapenzi ya Mungu inayale yote Mungu anataka ya timizwe zaidi kwetu, kama aliyo tuhadia.

598.Kwa sababu hili ni zuri, na la kukubaliwa mbele ya Mungu Mwokozi wetu ; anayetaka watu wote waokolewe na kupata kujua sana yaliyo kweli. (1 Timoteo 2 : 3, 4)

2) Mapenzi yake Mungu ina yale yote Mungu anataka tufanikiwe ao kama atufanikiwe, kufatana na ma amri yake.

599.Maana haya ni mapenzi ya Mungu, utakaso wenu, mwepuke na uasherati. (1Watesalonika 4 : 3)

3) Mapenzi ya Mungu ina yale yote Mungu anataka tuzidi ku ya vumilia na unyenyekevu kufuatana na kujuwa kwake.

600. Wakisimmamisha nafsi za wanafunzi na kuwaonya wakae katika imani, na kuwaambia ya kama kwa mateso mengi imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu. » (Matendo 14 : 22)
601. Halafu Yesu akawaambia wanafunzi wake : Mutu akuitaka kunifuata, ajikatae mwenyewe, achukue musalaba wake na kunifuata. (Matayo 16 : 24)

Ona tena Waebrania 12 : 6-11

**237. Nihali gani ya mwamini kufuatana na mapenzi ya Mungu ?**

1) Mwamini anakubali kwa maneno yote kua mapenzi yake Mungu sababu ni Mungu wake na Bwana wake na Mapenzi yake ni ya no mipaka.

602. Lakini mungu wetu ni mbinguni ; amefanya neno lo lote alilotaka. (Zaburi 115 : 3)
603. Maana mafikili yangu si máfikili yenu, wala njia zenu si njia zangu, Bwana nasema. Kwa maana kama vile mbingu ni juu sana kuliko dunia, hivi njia zangu ni juu sana kuliko njia zenu, na mafikili yangu juu kuliko mafikili yenu. (Isaya 55 : 8, 9)
604. akisema : Baba, ukipenda, uniondolee kikombe hiki ; lakini si mapenzi yangu yafanyike, ila mapenzi yako. (Luka 22 : 42)

2) Mwamini anakubali mapenzi yake Mungu sababu anajuwa kama Mungu wake ni mwema na rehema. Bwana huu anataka siku zote furaha, ata anapo mufikisha kwa majaribu na mahangaiko. Ana musubutisha, na kumufaridji na kumuokowa kwa wakati iposayo.

605. Ndiyo, hata nikipita kati ya bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa mabaya ; kwa Ukamaana wewe ni pamoja nami ; gongo lako na fimbo yako zinanifariji. (Zaburi 23 : 4)

606.Ukaniite sikuk ya mateso, nitakuokoa, nawe utanitukuza. (Zaburi 50 : 15)

607.Kwa maana nimejua kabisa ya kama wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala mamlaka, wala wenye uwezo, wala maneno ya sasa, wala maneno yatakayokuja, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kutumbe cho chote kingine hakitweza kututenga na mapendo ya Mungu yaliyo ndani ya Kristo yesu Bwana yetu. (Waroma 8 : 38, 39) .

3) Mwamini anakubali mapenzi yake Mungu sababu anajuwa kama Mungu wake ni mwenye hekima. Anaweza kugeuza mateso na majaribu kuwa baraka na kutufanya tena zaidi ya hiyo wanyenyekevu, mwenyi kutegemewa na zaidi ya shukrani. Ona sababu gani mateso, magonjwa na majaribu inaweza kuwako, katika mikononi mwa Mungu, kuwa shina ya baraka.

608.Nanyi, mulikusudi mabaya juu yangu, lakini Mungu alikusudi mema yafanywe, kama ni leo, kuponyesha uzima wa watu wengi. (Mwanzo 50 : 20)

609.Basi tukikwisha kuhesabiwa haki kwa njia ya imani, tuna salama kwa Mungu kwa njia ya Bwana yetu yesu Kristo ; kwa yeye vilevile tumepata njia ya imani kufikia neema hii tunayosimama ndani yake ; na tunafurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu. Wala, si hivyo tu, lakini tunafurahi katika mateso vilevile ; tukijua ya kwamba mateso yanafanya saburi, na saburi inafanya uvumilivu, na uvumilivu unafanya tumaini : na tumaini halipatizi haya ; kwa sababu mapendo ya Mungu yamemimiwa ndani ya mioyo yetu kwa njiya ya Roho Mutakatifu tuliyepewa sisi. » (Waroma 5 : 1-5)

**238. Nini inakuwa mupingana na mapenzi ya Mungu ?**

4) Ni mapenzi ya Shetani, ya ulimwengu na ya kiwili yetu, nikusema ni ya nia yetu mubaya.

610.Muwe na kiasi na kuangalia ; adui yenu Shetani, kama simba ya kunguruma anazungukazungaka akitafuta mutu amumeze. (I Petro 5 : 8)

611.Musipende dunia, wala maneno katika dunia. Mutu akipenda dunia, mapendo ya Baba si ndani yake. Maana kila kitu kilicho katika dunia, na tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kuburi cha uzima, havitoki kwa Baba lakini vinatoka kwa dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, lakini yeye anayefanya mapenzi ya Mungu anadumu hata milele. (I Yoane 2 : 15-17)

612.Kwa maana ninajua ya kwamba ndani yangu, maana, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema ; kwa sababu kutaka ni kwangu, lakini kufanya lililo jema siwezi. (Waroma 7 : 18)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 3 : 1-7: Mwandiko hii imeonesha mana gani dhambi ili ingiya duniani.

Luka 22 : 54-62: Wa adui wa Yesu wanatowa kwanguka kwa Petro.

Yoshua 7 : 18-22: Ma tamaa mubaya ya Akana imemupeleka ku maasi.

**239. Nini itupasayo kuomba ndani ya Baba yetu ?**

1) Tunaomba kama Mungu asimamishe na kuvunja mabaya ya nia ya kishetani, ya kiulimwengu na ya kimwili yetu. Ni kusema ya nia yetu mbaya.

613.Na Mungu wa salama ataponda Shetani chini ya miguu yenu kwa upesi. (Waroma 16 : 20)

2) Tunaomba pia kama Mungu anatupa nguvu na kutukomalisha ndani ya neno lake na ndani ya imani. Hivi tunaweza kwa wakati yote kufanya na furaha mapenzi yake, sawa wamalaika kule mbinguni.

614.Nanyi munalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mupate wokovu ulio tayari kufunuliwa kwa wakati wa mwisho. (1 Petelo 1 : 5)

615.Unitembeze katika njia ya maagizo yako; kwa maana ninapendezwa nayo. (Zaburi 119 : 35)

3) Basi, tunaomba kwa Mungu apate kutuchunga vema ata mwisho, hasa wakati tunapo uguwa.

616.Akaniambia : neema yangu inafaa kwako : kwa sababu uwezo wangu unakamolishwa katika uzaifu. Basi afazali sana nitajisifu katika uzaifu wangu, uwezo wa Kristo ukae juu yangu. » (2 Wakorinto 12 : 9)

617.Jaribu halikuwapata ninyi ila lililo kwa watu wote ; lakini Mungu ni mwaminifu, asiyewaacha ninyi kujaribiwa kuliko munavyoweza ; lakini pamoja na lile jaribu atafanya njia ya kukimbia, ili muweze kulivumilia. (1 Wakorinto 10 : 13)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 50 : 15-21: Mungu anazuiya niya mbaya ndugu ya Yosefu na amemupatia nguvu abakiye mwaminifu.
Yobu 1 : Mungu akumurusu Shetani kugusa imani ya Yobo.

**OMBI LA INE**

« Utupe sis leo chakula chetu cha kila siku »

Ina maana gani ?

Mungu analeta chakula kilasiku na kwa watu wote, ata na kwa wahuni, na bila hata tuki muomba, lakini tunaomba atufanie kujuwa mapenzi, juu tu mupokeye na roho ya shukrani.

Chakula cha kila siku inaelewa nini ?

Chakula cha kila siku inaelewa kusema chakula, mavazi, nyumba, shamba, Bivuko, hiiyote twapotayo kila siku jamaa ya nguvu, uongozi halali na watumishi wengi, kustahili ongozi wa kufaa wa kiserkali, na wakati nzuri amani, usawa, afia, sifa ya marafiki wenyi kufaa, ujirani kamili, na yote yapasayo kwa kuishi.

**240. Mungu anatupa chakula cha kila siku, hata na kwa wale awakuweza kumuomba na kwa hiyo ina mafaa gani tupate kumuomba ?**

Yesu anapenda sisi kuomba juu ya chakula cha kila siku, juu tujuwe kama ni zawadi ya Mungu, ni fazili isiyo mipaka. Chakula tunapo kula siku zote ni wingi wa neema inayotusaidia kwa kuishi siku kwa siku na haiko zawadi ya wa babu wetu ama ma roho ingine tunayo weza kueshimu juu yawo, haiko kwa ziaka kwa jibu ya kazi yetu, hii yote aya na maana kama Mungu hawa bariki. Vitu vyote viyema vya dunia hii ni zawadi ya mumbaji na Mungu wetu. Ndivyo yesu anatualika ndani ya Baba yetu kwa kumuomba chakula chetu cha kila siku, sababu anataka sisi tujifunze kwa kumupokea kwa moyo wa shukrani.

618. Macho ya watu wote yanakungojea ; nawe unawapa chakula chao kwa wakati wake. (Zaburi 145 : 15-16)
619. Kwa sababu ninawaambia ninyi, haki yenu isipopita haki ya waandishi na Wafarisayo, hamutaingia hata kidogo katika ufalme wa mbinguni. (Matayo 5 : 44, 45)
620. Mukishukuru Mungu ndiye Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo. (Waefeso 5 : 20)

## HISTORIA TAKATIFU

Luka 5 : 1-11: Simoni Petro alitumbuwa ya kwamba samaki alipata ilikuwa zawadi ya Mungu.

1 Wafalme 17 : Elia amemuombea kwa Mungu mwanamuke mjane, na uyu alitambua yakama Mungu alimubariki.

**241. Sababu gani tunasema « chakula chetu » ?**

3) Kama tukisema « chakula chetu » sababu hatuwezi kuomba kama juu ya chakula yenyewe tunakuwa nayo lazima. Tunapashwa tena kuomba juu ya chakula ya majirani wetu na kugawanya naye.

620. Kwa maana hata wakati tulipokuwa kwenu, tuliwaagiza ninyi neno hili : kama mutu hataki kufanya kazi, basi asile chakula. Maana tunasikia ya kwaba wengine wanatembea katikati yenu pasipo utaratibu, wasiofanya kazi hata kidogo, lakini wanajitia katika mambo ya wengine kazi kwa utulivu, na kula chakula chao wenyewe. (2 Watesalonika 3 : 10-12)

621. Lakini musisahau kutenda mema na kushirikiana na watu, maana sadaka kama hizi zinapendeza Mungu. (Waebrania 13 : 16)

**242. Sababu gani tunasema utupe leo « chakula chetu cha kila siku ?**

Tunasema « utupe leo chakula » na « chakula chetu cha kila siku » sababu imetupasa kya furahia yale yanayo kuwa faida kwetu kila siku inakuwa bazimu na kosa kwa kuuzunika juu ya kesho.

623. Na Bwana Mungu wako ataweka laana hizi zote juu ya adui zako, na juu yao wanaokuchukia, waliokutesa. Nawe utarudi na kutii sauti ya Bwana na kufanya maagizo yake yote niliyokuamuru leo. (Kumbukumbu 30 : 7-9)

624. Lakini tukiwa na chakula na nguo, kwa vitu hivi atatukana sisi vilevile. (1 Timoteo 6 : 8)

625. Basi musisumbukie ya kesho ; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Ubaya wa leo unafaa kwa leo. (Matayo 6 : 34)

626. Ni bule, ninyi munaoamka mapema na kukawia kwenda kulala, na kula chakula cha taabu : Yeye anamupa mupenzi wake usingizi. (Zaburi 127 : 2)

## HISTORIA TAKATIFU

Luka 12 : 15-21: Yesu amefundisha fumbo ya mulimaji anayefanya mavuno mzuzi na anaweka matumaini dani utajiri wake.

**OMBI LA TANO**

« Utusamehe deni, kama sisi vile vile tunavyosamea wadeni wetu »

Ina maana gani ?

Tunaomba Baba yetu aliembingumi asitazamie makoza zetu wala asitupie mbali maombi zetu, juu yayo, sababu hatuko wenyi kustahili kwa mema yake yote wala hatuya stahili. Lakini tunamuomba kwa yeye kuyakubalia kwa neema, sababu tuwatenda dhambi siku kwa siku na tunastaili malipizi. Ndjo maana inatupasa na sisi tusamehee kwa moyo wote hivyo itakuwa vema kwa wale wote wenyi kutukosea.

**243. Ndani ya ombi hii tunaomba nini ?**

Tunaomba Baba yetu wa mbingu asiyahesabie makosa yetu, lakini etusamehe tu kwa upendo wa Yesu Kristo.

627. Unirehemu, Ee Bwana ; Angalia mateso yangu ninayoteswa nayo nao wanaonichukia, umeninyanyua toka malango ya mauti. (Zaburi 9 : 13)
628. Na yule mutoza kodi alisimama mbali, hakutaka hata kunyanyua macho yake kwa mbingu, lakini alipiga kifua chake, akisema : Mungu unirehemu mimi wenye dhambi. (Luka 18 : 13)

**244. Sababu gani tuna musihi Mungu kutusamea ?**

Sababu tu watenda dhambi na kwelil waovu kwa mema yote tunayo yaomba kwake Munguna anatu yakubalia kila siku endayo. Tunastahili tu kwa ukweli mpaka malipizi.

629. Sistahili zo zote za rehema zako na za kweli yako ulioonyeshea mutumishi wako ; kwa maana na fimbo yangu nilivuka Yorodani huu ; na sasa nimekuwa vikosi viwili. Uniponyeshe, ninakuomba, kwa mukono wa ndugu yangu, kwa mukono wa Esau, kwa sababu ninamwogopa asije na kunipiga, mama pamoja na watoto. (Mwanzo 32. 10, 11)
630. Yule mwana akamwammbia : Baba, nimefanya dhambi juu ya mbingu na mbele yako, sistahili tena kuitwa mwana wako. (Luka 15 : 21)

**245. Tunamushukuru je Mungu juu usamehe anaye tu kubalia ?**
Tuanyahidi kusamea kwa moyo wetu wote kwa wale wenyi kutukosea. Natunawaidia pia kuwa famia nawo vizuri.

631. Kisha Petro akamukwendea akamwambia : Bwana, ndugu yangu anikosee mara ngapi nami nimusamehe ? hata mara saba ? (Matayo 18 : 21, 22)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 22: 1-19: Mungu amemujaribu Abrahamu na kusabitisha imani yake.

**246. Kitokeo gani itafikia yule aombaye uruma kwa Mungu lakini asiyekua na nia pia ya kusamehe majirani wake ?**
Mungu hatkubali kusamehe yule hataki pia kusamehe majirani, mwenye kulaini tu, ombi lake itamuletea asira ya Bwana.

632. Mukisimama kuomba mukiwa na neno juu ya mutu, sameheni ; ili Baba yenu aliye mbinguni awasamehe ninyi makosa yenu. (Lakini kkama ninyi hamusamehe, Baba yenu aliye mbinguni, hatawasamehe ninyi makosa yenu.) (Marko 11 : 25, 26)

## HISTORIA TAKATIFU

Matayo 18 : 21-35 : Hapa Yesu anazungumuzia katika fumbo haliya mutumishi moja asiye kuwa na huruma aliye kataa kuhurumia mwenzake deni aliyo kuwa naye rafiki wake. Japo Bwana wake aliweza kumwachilia deni kubwa aliyekuwa nayo kwa Bwana wake.
Na hii andiko inatufundisha kama imetupasa kujuwa kusamehea majirani wetu kama vile Mungu anatusamehee.

**OMBI LA SITA**

« Na usitulete katika majaribu »

Ina maana gani ?

Mungu hawezi kujaribu mutu lakini tunamuomba kwa yeye kutuchuga na kutushindia, ila la shetani, ulimwengu na hali yetu mubaya inapenda kutusukuma kupitia uwongo yao na kwangusha wengi kukosa kwamini Yesu na kutuingiza mu kukata tamaa ao mu mabaya mengi ya nguvu. Na kama majaribu inatufikia, tunaomba mungu kutusaidia kwa kuya shinda.

**247. Uyaoneshe maana mawili ya « jaribu »?**
Neno « jaribu » inaonesha kujaribiwa kwa imani yetu itokayo kwa Mungu, ao kazi ya shetani inayo tushawishi sisi kufanya ubaya.

**248. Munia gani Mungu anaweza kujaribu mutu ?**
Mungu anajaribu watoto wake anapima kwa kuona atua ya imani na anfanya hivyo kwa kumutakasa na kumusimamisha imara.

633. Basi Yesu aliponyanyua macho yake akaona makutano makubwa wanakuja kwake, akamwambia Filipo; tununue mikate wapi, hawa wapate kula ? Alisma maneno haya amujaribu, kwani alijua mwenyewe atakayoyafanya. (Yoane 6 : 5,6)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 22 : 1-19 : Mungu alipima Abrahamu kwa kuona na kumusimamisha nguvu ndani ya umani

Marko 7 : 24-30 : Yesu anajaribu mwamini juu apate kukpima na kumusimamisha ndani ya imani.

**249. Yaoneshe maana ya neno « jaribu » nadani ya ombi la sita iliyo ndani yaombi ya « Baba yetu ».**

Ndani yaombi la sita ya Baba yetu, neno « jaribu » inaonesha kujaribiwa kwa ubaya.

**250. Tunajaribiwa wakati gani katika ubaya ?**

Tunajaribiwa katika ubaya wakati shetani, dunia ao ma nia yetu mbaya, matendo inayo tusukuma kwa kuto kuamini Yesu na kwa kupoteza matumaini ya maisha ya milele, ao kwa kuishi ndani ya dhambi. Watumia uwongo na vitu vya kutowezesha na kutusukuma kwa maovu ao kwa nia yote ya dhambi.

634.Mutu akijaribiwa, asiseme : ninajiribiwa na Mungu : maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hajaribu mutu. Lakini kila mutu anajaribiwa kivutwa na kudanganywa na tamma yake mwenyewe. (Yakobo 1 : 13, 14)

635.Ole wa dunia kwa sababu ya mambo ya kukosesha ! Kwa maana sharti mambo haya yafike ; lakini ole wa mutu yule anayeyaleta ! (Matayo 18 : 7)

636.Muwe na kiasi na kuangalia ; adui yenu Shetani, kama simba ya kunguruma anazungukuazunguka akitafuta mutu amumeze. (1 Petelo 5 : 8)

637.Mwana wangu, kama wenye dhambi wakikushawishi, usikubali. (Mezali 1 : 10)

638.Maana Dema aliniacha, akiwa amependa dunia hii ya sasa, na alikwenda hata Tesalonika ; Kreske kwa Galatia, Tito amekwenda Dalmatia. (2 Timoteo 4 : 10)

## HISTORIA TAKATIFU

Mwanzo 3 : Ewa anajaribiwa na anakatala kutii torati la Mngu.

Matayo 4 : 1- 1 : Satana anamujaribu Yesu na anataka kumutia katika dhambi.

Yoane 13 : 1 – 2: Satana anamujaribu Yuda kwa kumutoa Yesu.

Matayo 27 : 3 – 5: Yuda amekufa kwa kupoteza matumaini. Alizania ya kwamba dhambi zake ilikuwa mkubwa ili Mungu apate kumusahea.

Luka 22 : 54 – 62: Satana amemujaribu Petro kwa kumukataa Yesu.

2 Samueli 11 : 1- 12 ; 25: Daudi amejaribiwa kwa ali zake mutenda maovu kwa kusharautika na kuua.

**253. Ndani y ombi ya Baba yetu tunaomba nini ju ya jaribu ?**

1) Tunaomba kwa Mungu etukinge na kutuokowa ju tusikafikie kujaribiwa na kufanya ubaya.
   639.Lakini Bwana ni mwaminifu, atakayewasimamisha ninyi, na kuwalinda ninyi na yule mwovu. (2 Watesalonika 3 : 3)

2) Tunaomba kwa Mungu ku kazisha imani yetu japo wakati anaye ruhusu tujaribiwe, ju tuwe wa kushinda wakati wote.

   640.Jaribu halikuwapata ninyi ila lililo kwa watu wote ; lakini Mungu ni mwaminifu, asiyewaacha ninyi kujaribiwa kuliko munavyoweza ; lakini pamoja na lile jaribu atafanya njia ya kukimbia, ili muweze kulivumilia. (1 Wakorinto 10 : 13)
   641.Kwa hivi twaeni silaha zote za Mungu, mupate kuweza kushindana katika siku ya uovu, na mukikwisha kutimiza yote, kusimama. (Waefeso 6 : 13)

**OMBI LA SABA**

« Utuokoe na yule mwovu »

Ina maana gani ?

Kwa kifupi ju ya neno hii, kila ombi tuombao kwa Baba wa mbingu. Tuna muomba kwa kutowa na mabaya yote iwezakanapo kutufikia ku mili yetu na ndani ya moyo wetu, mu vitu vyetu na mu furaha yetu, hivyo tunaomba kwa Mungu atukubalie kwa siku yetu ya mwisho kifo ya salama, kwa kutupitisha ndani ya bonde ya kwali ya mauti kufika kule kusike mbinguni.

## 252. Tunaomba nini wakati tuombapo hivi ?

1) Tunaomba kwa Mungu kwa kututia ku ukiago ya ubaya wote. Ju ni yeye pekee ana weza kutokowa hiyo ni kwake pekee umetufaa kumuomba. Wababu na mapepo ya kiasili haweko ata nauwezo lolote ya kuyafanya. Hivi aina sababu tuyaombe wale wengi kuwagekia wakati wanapo kuwa ndani ya magumu, wana wafania ibada, ila Mungu pekee anastahili. Wana kufuru Bwana kwa namna hii.

642.Mabaya hayatakupata wewe wala tauni haitafika na hema yako. (Zaburi 91 : 10)

643.Uisnifichie uszo wako, usiondoe mutumwa wako na kasirani. Umekuwa musaidia wangu, usinitupe wala kuniacha, Ee Mungu wa wokovu wangu (Zaburi 27 : 9)

644.Sanamu zao ni feza na zahabu, kazi ya mikono ya watu. Zina vinywa, lakini haziseme, zina macho, lakini hazioni ; zina masikio, lakini hazisikii ; zina pua, lakini hazinusi ; zina mikono, lakini hazitembei ; wala hazitoi sauti kwa koo yao wao wanaozifanya watakuwa sawasawa no ; ndiyo, kila mutu anayezitumainia. Ee Israeli, utumainie Bwana (Zaburi 115 : 4 – 9)

2) Tunaomba tena kwa Mungu epushe kwetu, kufuatana na mema yake, majaribu tunayovumilia, na yote yanayotuangaisha. Tunayafanya na tumaini yote, sababu alihaidi kwa kuwa

musaidizi. Kama hayo haiko mapenzi yake, tunamuomba kwa kutusaidia kwa kuvumilia magumu yetu kufikia kwa uzuri.

645.Wakisimamisha nafsi za wanafunzi na kuwaonya wakae katika imani, na kuwaambia ya kama kwa mateso mengi imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu. (Matendo 14 : 22)

646.Maana yeye Bwana anyemupenda, anamutakasa kwa mateso, Naye anapiga kila mwana anayemupokea (Waebrania 12 : 6 )

647.Akaniambia : Neema yangu inafaa kwako : kwa sababu uwezo wangu unakamilishwa katika uzaifu. Basi afazalil sana nitajisifu katika uzaifu wangu, uwezo wa Kristo ukae juu yangu. (2 Wakorinto 12 : 9)

648.Atakuokoa na mateso sita ; ndiyo, na katika saba ubaya hautakugusa. (Yobo 5 : 19)

649.Na saburi inafanya uvumilivu, na uvumilivi unafanya tumaini (Waroma 5 : 4)

650.Kwa maana ninahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama tukiyafananisha na utukufu ule ukakaofunuliwe kwetu. (Waroma 8 : 18)

3)Tuanomba mara tena Mungu kwa kutuokowa siku moja kwa mabaya yote kutukubalia kwa kifo ya salama. Yeye pekee anaweza kufanya yote yale kwa kutusaidia kwa kufa ndani ya imani katika Yesu Kristo Mwokozi. Kwa hiyo, ni ju tu kwa imani katika Kristo tunafikia kupata usamahae wama kosa na uzima wa milele.

651.Bwana ataniokoa na kila neno baya, na kunichunga hata nifike kwa ufalme wake wa mbingu : kwake utukufu uwe kwa milele na milele. Amina. (2 Timoteo 4 : 18)

652.Sasa, Bwana, uruhusu mutumishi wako aende kwa utulivu kama ulivyosema, kwa sababu macho yangu yameona wokovu wako. (Luka 2 :29-30)

653.Kwa maana kwangu kuishi ni Kristo, na kufa ni faida. Lakini ikiwa kama kuishi katika mwili, haya ni matunda ya kazi yangu, sijui nitakalolichagua. Lakini ninasongwa katika

654.mambo mawili, nikitamani kwenda zangu nikae pamoja na Kristo ; maana ni vizuri zaidi sana (Wafilipo 1 : 21 – 23)

655.Nyumba ya haya nimewekwa taji ya haki, Bwana muhukumu wa haki atakayonipa siku ile ; wala si mimi tu, lakini watu wote pia waliopenda kuonekana kwake. (2 Timoteo 4 : 8)

**251. Kwa mwisho ya yote tunahakikisha nini kwa Baba yetu ?**
Tunaakikisha kama Mungu ni yeye pekee aliye Mufalme .

1) Na ni kwa yeye kunatokea masidizo yote

2) Tuankikisha kama yeye pekee anakuwa na uwozo wa kujibia kwa maombi yetu

3) Tunakikisha kwa yeye pekee anakubaliwa kwabu diwa na sifa kwa yote anayo fanya juu yetu.

**KWA KIFUPI**

« Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu hata milele amina. »

Inamana gani neno « Amina » nikusema ?

« Amina » Inashuhudia ukweli yale Baba wa Mbingu anye furaia maombi yetu nakuyasilikiliza. Ni yeye pekee, anayeturuhusu kwa kuomba hivyo na alia hadia kwa kuisikiliza « Amina Amina » inasema hivi ndiyo, ndiyo, ifanika hivyo hivyo.

✞✞✞

## SURA YA NNE

## UBATIZO

## MASACRAMENTI

**257. Sakramenti ni nini ?**
Kunakuwa vitu tatu ya lazima ju kufanike sakramenti :

1) Sakramenti ni kitendo kienyi kutakaswa yale Mungu pekee alisimamisha.

2) Sakramenti ni kitendo kienye kutakaswa ndani yake muna sauti ya Mungu yenyi kujiunga kwa viombo isionekana .

3) Sakramenti ni kitendo yale Mungu anatukabizia na kututumanisha usamehe ya dhambi yale Yesu alichukuwa kwa kujitowa kwake.

**258. Kuna aina ngapi ya ma sakramenti yenyi kufananisha na hiyo ?**
Kuna ma sakramenti mawili, Ubatizo na Meza ya Bwana

**1. NDIYO UBATIZO**
Ubatizo ni nini ?

Ubatizo siotu maji ya kanuni, lakini maji yenyi kutengenezwa kufuatana na amri ya Mungu na kulingana na neno lake.

Na sauti hii ya Mungu ni je ?

Bwana wetu je tu Kristo ku bana ya mwisho ya Matayo mutakatifu : "Mwende katika mataifa wote muwafanye kuwa wafuasi, mu kiwa batiza kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mutakatifu."

**256.Neno kubatiza neno ya kigreki ina maana gani ?**

Neno kubatiza inasema kutumia maji kwa kuosha kitu fulani . Wanaweza kufunja hiyo kwa kuosha kumuangia na kutumbukiza.

655. Tena wakitoka sokoni, wasiponawa hawakuli. Na walilpokea maneno mengi mengine na kuyatii, kama kuosha vikombe, na vyungu, na vyombo vya shaba. (Marko 7 : 4)
656.Basi sasa, unakawia nini ? Simama ubatizwe, usafishe dhambi zako, ukiitia jina la Bwana. (Matendo 22 : 16 )
657.Kweli mimi ninawabatiza ninyi kwa maji hata toba ; lakini yeye anayekuja nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, na sistahili hata kuchukua viatu vyake ; yeye atawabatiza ninyi kwa Roho Mutakatifu na kwa moto. (Matayo 3 : 11)

**257.Sababu gani ubatizo aiko tu maji ya bure ?**

1) Ubatizo si majitu ya bure sababu tunayo tumia kufunatana na amri ya Mungu.

2) Ubatizo sikama maji tu ya bure sababu tuna ya tumia kunjina la Baba, la Mwana na la Roho Mutakatifu. Maji ya ubatizo inaunganisha katika sauti ya Mungu.

**258.Nazni aliye amuria ubatizo uwe ?**

Ni Mungu pekee aliye amria ubatizo iwe, hivyo Yesu Mwana wa Mungu akaruhusu kwa kanisa kwa kubatiza watu wa kila taifa.

658.Yesu akakuja kwao, akawaambia akisema : nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwendeni basi mukafanye matayifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakatifu. (Matayo 28 : 18 – 19)

**259.Ni kwa nani ubatizo unafanikwa ?**

Ni kwa makanisa ubatizo unafanikwa kupitia wa chungaji wake, lakini kwa wakati wa shida ya haraka ao Mushinda kupita

wachungaji, kila mwaminifu anakuwa na mamulaka ya kuweza kubatiza. Tazama mfano mpupi ya ubatizo mwisho ya kitabu hii.

659.Mutu atuhesabu sisi hivi, kama watumishi wa Kristo na mawakili ya siri za Mungu. (1 Wakorinto 4 : 1)

**260.Ina mana gani usemi « Kubatiza » kwa juna la Baba, la Mwana, na la Roho Mutakatifu ?**

Hii muti inasema hivyo, kuspitiya kwa ubatizo tunapokeya katika unganisho ya utatu mutakatifu.

**261.Nani wa kuweza kubatiziwa ?**

Yesu anasema kwetu kwa kubatiza watu wa taifa yote. Waume na wanawake, wazee, wakubwa na vijana na pia watoto wachanga. Kakuna ata mumoja anayetengwa kubatiza.

**262.Achanisho gani tufanyapo katika kubatizo ?**

1) Watoto wanabatiziwa kwa ombi ya wazazi wake ao kwa kila mtu anye kuwa na mamlaka ju yao.

661.Nanyi baba, musichokoze watoto wenu ; lakini muwalee katika azabu na maonyo ya Bwana. (Waefeso 6 : 4)

2) Wale wanaoweza kufundishiwa ju ya imani wanabatiziwa kisha kupokea mafundisho katika uketo wa mafundisho ya Biblia.

662.Nao waliopokea neno lake kwa furaha wakabatizwa ; na sikku ile wakazidishwa watu kama elfu tatu. (Matendo 2 : 41)

**263.Watu wengi wanahakikisha kama si lazima kubatiza watoto. Hii hali ni kinyume ya mafundisho ya Biblia. Je tunaweza kuakikisha kama tunaweza kubatiza tena watoto ?**

1) Inafai kubatiza watoto sababu nawo pia waunfunya kuwa kipande« yamataifa ».

663. Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakatifu. (Matayo 28 : 19)

664. Petro akawaambia : Tubuni mukabatizwe kila mumoja kwa jina lake Yesu Kristo, mupate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mutapokea zawadi ya Roho Mutakatifu. Kwa sababu ahadi hii ni kwa ajili yenu, na watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu. (Matendo 2 : 38 – 39)

2) Watoto nawo pia ni wenyi zambi mbele ya Mungu. Ndivyo kanuni inafundishwa, dhambi ya asili. Hivi inafai ku wabatiza ju wafikie nao kupata usamehe na wokovu wa Yesu Kristo. Ubatizo unawabadirisha ju ya uzima wa milele.

665. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi ; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. (Zaburi 51 :7)

666. Wakamuletea watoto ili awaguse ; na wanafunzi waliwakemea. Yesu alipoona, alichukizwa sana, akawaambia : acheni watoto wadogo waje kwangu, musiwazuize, sababu ufalme wa Mungu ni wao.Kweeli ninawaambia ninyi, Mutu asiyepokea ufalme wa Mungu kama mutoto mudogo, hataingia kule, hata kidogo. (Marko 10 : 13 – 15)

667. Yesu akajibu ; kweli, kweli ninakuambia, Mutu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwilil ni mwili ; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. (Yoane 3 : 5 – 6)

3) Inafai kubatiza watoto sababu Biblia inakikisha kama wanaweza kuamini nao pia na ubatizo ni namna kubadirisha. Inafanisha upya kwa uzima wa milele kwa imani katika Yesu Kristo..

668. Lakini kila mutu anayekosesha mumoja wa wadogo haw<a wanaoniamini, inafaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, apate kuzama kilindini mwa bahari. (Matayo 18 : 6)

669. Yesu alipoona, alichukizwa sana, akawaambia : acheni watoto wadogowaje kwangu, musiwazuize, sababu ufalme wa Mungu ni wao. Kweli ninawaambia ninyi, Mutu asiyepokea ufalme wa

Mungu kama mutoto mudogo, hataingia kule, hata kidogo. (Marko 10 : 14 – 15)

670. Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyafanya lakini kwa rehema yake alituokoa, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa mupya na kufanywa upya na Roho Mutakatifu ; ndiye aliyemwanga juu yetu, kuzidi sana, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu ; tulihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa wariti kwa tumaini la uzima wa milele. (Tito 3 : 5 – 7)

**264. Wazamini(Wasimamizi) wakike ao kuime ni wa nani na sababu gani Eklezia iliruhusu kuwe uzami ni hiyo ?**

Wazamini(Wasimamizi) ni mwamini aney kuwa na kazi ya ya kusimamia watoto kwa ubatizo na kuchunguza kwa mwenendo wa ukristo wake. Wazamini(Wasimamizi) wa kike ni mwamini ni vilevile anaye fanya kazi sawa sawa hawa kuime, Mtoto anaye kuwa na wazamini(Wasimamiszi) wa kiume ao wa kike anye chunguza kwa mwenendo wa imani anaitwa pia Mwangalizi wa kike ao mume.

Na makazi ya wazamini(wasimamizi) na wazamini (Wasimamizi) wa kike ndiyo ufuatoyo :

1) Weko wa shuuda wa ubatizo na wanaweza kwa wakati wote kwakikishia kwa uchunguzi wao kama walibatizwa kufuatana na undowa wa Mungu.

   671. Lakini kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mutu mumoja ao wawili ili kwa vinywa vya washuhuda wawili ao watatu kila neno lisimamishwe. (Matayo 18 : 16)

2) Wanapashua kuchunguza kwa mwenendo kwa mwenendo wa mtoto, hasa kama ni mwenye kupokea na wazazi wake.

3) Wanalazimishwa kumuombea yule

## 2. UZARIWA YA UBATIZO

Nini ifanikao katika ubatizo

Ubatizo inaleta usamaa wa zambi. Inafungua kwa kifo na kwa Shetani na inaleta wokovu kwa wote waminio, kufuatana na sauti na magizo ya Mungu.

Maagizo ya Mungu na sauti yake ni je ?

Bwana wetu Yesu Kristo anasme ku maandiko ya mwisho ku baruwa ya Marko mutakatifu « Atakaye amini na kubatiziwa ataokolewa, lakini asiye amini ainekulsha kuhu kuniwa »

**265. Ni matendo mema gani makubwa yanasamehewa ju ya ubatizo ?**

1) Ubatizo inaleta usamehe wa dhambi.

672. Petro akawaambia : Tubuni mukabatizwe kila mumoja kwa jina lake yesu Kristo, mupate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mutapokea zawadi ya Roho Mutakatifu. (Matendo 2 : 38)
673. Basi sasa, unakawia nini ? Simama ubatizwe, usafishe dhambi zako, ukiitia jina la Bwana. (Matendo 22 : 16)

674. Maana ninyi wote ni wana wa Mungu, kwa imani, katika yesu Kristo. Maana ninyi wote muliobatizwa na kuingizwa katika Kristo, mumevaa Kristo. (Wagalatia 3 : 26 - 27)

2) Ubatizo unaokowa kifo na Shetani

675. Ao hamufahamu, sisi sote tuliobatizwa katika yesu Kristo, tulibatizwa katika kufa kwake ? (Waroma 6 : 3)

3) Ubatizo inaleta wokovu wa milele

676. Naye aliwaambia : Musishangae, munatafuta Yesu wa Nazareti aliyesulibiwa ; amefufuka, hauyo hapa. Tazama pahali walipomuweka. (Marko 16 : 6)

677. Mufano wa maneno haya ni ubatizo unaowaokoa ninyi sasa, si kuondosha uchafu wa mwili, lakini jibu la zamiri safi mbele ya Mungu, kwa njia ya ufufuko wa yesu Kristo. (1 Petro 3 : 21)

**266. Kama Yesu aliweza kutukubalia mema haya yote, sababu gani inafai tena ubatizo ?**

Ni kweli kama Yesu alitukubalia mema yake yote, kupitia mateso na kifo yake. Lakini Mungu aliweka ma namna kwa kuwa Roho Mutakatifu anatujulisha. Itwayo namna ya neema. Inakuwa ma namna tunayo pokea neema ya Mungu na yale yote Yesu aliye tukubalia. Ni tatu tu : Neno la Mungu namuna yake.

678. Maana ninyi wote ni wana wa Mungu, kwa imani, katika yesu Kristo. Maana ninyi wote muliobatizwa na kuingizwa katika Kristo, mumevaa Kristo. (Wagalatia 3 : 26 – 27)

679. Na wengine kwenu mulikuwa hivi ; lakini mulioshwa, lakini mulitakaswa, lakini mulihesabiwa kuwa na haki katika jina la Bwana yesu, na katika Roho ya Mungu wetu. (1 Wakorinto 6 : 11)

**267. Ubatizo inagabiza mema haya yote kwa nani ?**

Ubatizo inagabiza mema haya yote kwa wale wenyi kwamini. Ndiyo Biblia isemavyo.

680. Anayeamini na kubatizwa ataokolewa ; asiyeamini atahukumiwa. (Marko 16 : 16)

**268. Bila ubatizo tunaweza kuokolewa ?**

Ndiyo, tunaweza kuokolewa bila kulakubatiziwa, wakati hatukuweza kupata sakramenti. Ila tu imani ni ya lazima sana kwa kupata wokovu. Maana yoke yeyote anaye kufa katika imani ana uzima wa milele. Lakini mtu akazarau hii sakramenti na kukataa kubatizwa, anaonesha kama ana na imani moyoni mwake.

## HISTORIA TAKATIFU

Luka 7 : 29 – 30 : Wafarisayo na walimu wa sheria wana hukumiwa kwa sababu ya kutoeshimiya Ubatizo
Luka 23 : 39 – 43 : Mumuja wa wale watnda mabaya waliotundikwa pamoja na Yesu ana okolewa, bila Ubatizo, kwani anakuwa na imani muko Yesu Kristo.

**3. MA NUFAA YA UBATIZO**

Je maji inweza kufanya vitu vikubwa hivyo ?

Si maji tu, kweli, inaweza kufanya vitu vikubwa, lakini ni neno la Mungu inayo unganisha maji kwa imani inayo shindilia katika neno hii ya Mungu katika maji. Na bila neno la Mungu, maji hayo ni maji tu kama maji ya bure. Ni kusema ni maji ya Baraka na ya uzima, kiosho kinayo tufunya kuzalikwa katika Roho Mutakatifu. Ndivyo mitume Paulo na Tito waliosema kubaruwa ya tatu.
Alituokowa, si ju tuliweza kufanya matendo mema ya ha ki, lakini kufuatana na mema yake pekee, kwa kiosho ya mabadiriko na upya ya Roho Mutakatifu.
Aliweka ju yetu kwa wingi kwa neema yake, sisi tu wariti katika tumaini ya uzima wa milele ». Na hii neno ni hakika kweli

**269.Kwa kupitiya kwa ubatizo je tunaweza kupata usamehe wa dhambi kufunguliwa kwa kifo na Shetani na wokovu wa milele ?**

Neno la Mungu inaunganisha mibaraka makubwa kupitia kwa maji ya ubatizo anayatiliya sawa hivyo. Na imani inayo fanika kwa mahandio ndani ya Neno la Mungu inatia usamaa, uzima na wokovu ipatikanayo ndani ya sakramenti.

681.Waume, mupende wake wenu, kama vile Kristo alivyopenda kanisa, na kujitoa mwenyewe kwa ajili yake; apate kulitakasa, akiwa amelisafisha kwa maji latika neno (Waefeso 5 : 25 – 26)

**270.Sababu gani Biblia inasema kama ubatizo ni kiosho ya kufanika upya katika Roho Mutakatifu ?**

Ni sababu kupiya ubatizo Roho Mutakatifu inatufanya kupya, kuamisha na kushindilia imani katika moyo. Kwa imani hiyo, tunafikia kwa mema itokayo kwa Yesu yenyi kutiliwa ndani ya ma

ya ubatizo, ndiyo Roho Mutakatifu inafanya kupya anye kubatizwa kufikia uzima mupya katika Yesu Kristo.

**4. MAANA YA UBATIZO**

Ubatizo ina maana gani ndani ya uzima ya mukristo ?

Ubatizo ina maana kusema uzima ya mtu wazamani inayo kuwa kwetu wapashwaiza mishwa uzuni na kitubio ya kila siku. Inapashwa zaidi tena ife ndani ya dhambi na mania yake yote mbaya. Na kwa kila siku piya, mtu wa sasa anapashwa azalike kwetu, mtu mwenyi kuishi kwa lote ndani ya ukweli na utakaso mbele ya Mungu.

Imeandikwa wapi haya yoté ?

Mutume Paulo anandikiya Waroma kubaruwa ya zita « Tulizikwa naye katika kufa kupitia kwa ubatizo, ju kwa kuwa, vile Kristo alifufuka katika wafu kwa sifa ya Baba, hivyo sisi wote tnaishi ndani ya uzima mupya.

**271. Umutu wazamini ina mana gani ?**

Wakati Adamu alipo kosa kwa amri ya Mungu, umbo wake ulibadirika kabisa, ulikuwa mbele na safi, lakini ubabao lirika mbaya. Takatifu ya kukataliwa na yenye makosa, ndiyo umbonde ili kataliwa tuliiga kwa Adamamu sisi wote : Ndiyo utuayo mtu wazamani.

682. Mwondoshe, kwa maneno ya mwenendo wenu wa mbele, yule mutu wa zamani, anayeharibika kwa kufuata tamaa za udanganyifu. (Waefeso 4 : 22)

**172.Namna gani tunaweza kuosha umutu huu wazamani ?**

Tunaweza kushaweza kuosha umutu huu wazamani kwetu kupita kwa kuuzunika na kutubia kwa kila siku. Tu kiuzunika ju ya dhambi zetu ao tukizitubu, tunaweza kwa nguvu tulio pata katika ubatizo na kwa uwezo ya Roho Mutakatifu inayotunika kwetu, kushinda kabisa kabisa ku vishawishi na kuubaya.

683. Nao walio watu wa Kristo wamesulibisha mwili pamoja na mawazo mabaya na tamaa mabaya. (Wagalatia 5 : 24)

**273. Umutu mupya ni nini ?**
Umutu mupya ni upya waumba yani Roho Mutakatifu alitufanya kuzalikwa kwetu kwa njia ya ubatizo itupelekao kuishi maisha mapya katika imani katika Yeu Kristo.

684.Na kuvaa yule mutu mupya aliyeumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli. ( Waefeso 4 : 24)

**274.Umutu mupya unazalika je kwetu kwa kila siku ?**
Umutu mupya uzalika kwetu wakati Mungu anatupatia nguvu ya kupinga kwa dhambi na kuishi kufuatana na neno lake.

685.Na kuvaa yule mutu mupya aliyeumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli. (Waefeso 4 : 24)

**260. Kwa hiyo kazi ya ubatizo ni nini ?**
Katika ubatizo tunairiaba Kristo. Sawa mukristo mwenyi kubatizwa na tunaitwa siku kwa siku,kwa kurudilia kwa ubatiza watu. Sababu inakuwa chemchem ya Yesu liweza kkutgabizia. Tunatenda kwa kila siku ubaya, kwa njia ya kutubia. Tunafikia kupata neema na usamehe tulio pokea ndani ya sakramenti. Twapatiyamo tena nguvu ya kuepuka makosa na kutembeya ndani ya maisha mapya katika imani na utiifu.

**261. Tunakataa nini katika mwisho yetu yote kwa kupata ubatizo ?**
Kwa kupata ubatizo, tu nakataa Shetani na matendo yake yote.

**262. Kwa kupata ubatizo tunagizwa nini ?**
Kwa kupata ubatizo, tunahaida kwa kuwa wake wote kwa Mungu pekee na wakweli na kwa kunutumikia.

**263. Mukristo anarusilia tena kuapa kwake wakuti gani yale aliefanya na Mungu wakati wa kubatizwa ?**
Mukristo anarudiliatena hii kuapa ni kwa siku kwa siku ya uzima wake.

✞✞✞

# SURA YA TANO

## HUDUMA YA FUNGULO NA UKIRI

### 1. HUDUMA WA FUNGUO

Huduma wa funguo ni nini ?

Ni uwezo wa kipekee Bwana Yesu Kristo aliyotoa kwa kanisa duniani. Anawasamehe wenye dhambi na wenye kuomba musamaha na kukataa kuwasamehe wasioadibishwa, wakati wowote wanapo fanya mioyo yao kuwa mugumu.

Imeandikwa wapi ?

Imeandikwa kutoka injili ya Mutakatifu Yoane , sura yake 20:23 : "Yesu Kristo akapuliza juu yao, akawambia : Mpokee Roho Mtakatifu, wowote mutakao wasamehe dhambi, zinasamehewa kwao, na wale musiosamehe hawatasamehewa."

**259. Ni uwezo kani ya Uduma wa funguo?**
Uduma wa funguo inakuwa na uwezo wa kuhubiri Neno la Mungu, kutoa utakaso na ondoleo ao namna ingine ya kuzuria dhambi.

686.Lakini ninyi ni taifa chaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio mali ya Mungu mwenyewe, mupate kutangaza uzuri wake aliyewaita ninyi toka giza mwingie katika nuru yake ya ajabu(1 Petro 2:9)
687.Akawaambia: Kwendeni katika dunia pia, mukahubiri Habari Njema kwa kila mutu.(Marko 16: 15)
688.Yesu akakuja kwao, akawaambia akisema: Nmepewa mamlka yote mbinguni na duniani. Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakatifu(Matayo 28: 18 – 20)
689.Naye wakati alipokwisha kusema maneno haya , akawapulizia, akawaambia: Mupokee Roho Mutakatifu. Wo wote mukiwasamehe dhambi, zinasamehewa kwao, na wo wote mukiwafungia dhambi zinafungwa kwao(Yoane 20: 22 –23)

690.Kweli ninawaambia ninyi, Vitu vyo vyote munavyofunga duniani vitafungwa mbinguni; na vitu vyo vyote munavyofungua duniani vitafunguliwa mbinguni. (Matayo 18: 18)

**254. Kwanini tunaita huu uwezo "Uduma wa unguo"?**

Huu uwezo unaitwa "Uduma wa funguo" kwasababu unafungua mbingu kwa wenye dhambi wenye kutubu kwa kuwaondolea dhambi, na kuwakatalia wenye kufanya mioyo yao mizumu ya dhambi ondoleo ya dhambi.

691.Nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani litafungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litafunguliwa mbinguni. (Matayo 16: 19)

**255. Kwa nini Uduma wa funguo ni uwezo "wa kipekee" wa kanisa?**

1) Uduma wa funguo ni uwezo " wa kipekee" wa kanisa, kwasababu ni uwezo wa na sio kwa sada kiroho.
2) Uduma huu ni wa kipekee kwa kanisa kwasababu ni kwa yale tu Yesu aliuleta alikwaminisha

**256. Nani Yesu alikwaminisha uduma wa funguo?**

Yesu ali kwaminisha uwezo wa funguo kwa kanisa lake ulimwenguni. Akauleta kwa kila mwaminifu na kwa kila mtaa.

692.Hamujafahamu bado, wala hamukumbuki mikate mitano ya watu elfu tano, na vitunga vingapi mulivyookota? (Matayo 16: 9)

693.Naye wakati alipokwisha kusema maneno haya, akawapulizia, akawaabia: Mupokee Roho Mutakatifu. Wo wote mukiwasamehe dhambi, zinasamehewa kwao, na wo wote mukiwafungia dhambi, zinafungwa kwao. (Yoane 20: 22-23)

694.Lakini ninyi ni taifa chaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio mali ya Mungu mwenyewe, mupate

kutangaza uzuri wake aliyewaita ninyi toka giza mwingie katika nuru yake ya ajabu (1 Petro 2:9)

695.Naye kama akikataa kuwasikia, ambia kanisa; na kama akikataa kusikia kanisa vilevile, awe kwako kama mutu wa mataifa na mutoza kodi. Kweli ninawaambia ninyi, Vitu vyo vyote munavyofunga duniani vitafungwa mbinguni; na vitu vyo vyote munavyofungua duniani vitafunguliwa mbinguni. Ninawaambia ninyi tena, ya kwamba wawili katikati yenu watakapopatana duniani kwa kitu cho chote watakachoomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa pahali watu wawili ao watatu wanapokusanyika kwa jina langu, mimi ni pale katikati yao.(Matayo 18: 17-20)

**283.Nani anaweza kuodolewa dhambi?**

Wanaweza kuondolewa dhambi mwenye kutubu.

696.Tubuni basi, mugeuke, ili dhambi zenu zuiondoshwe, zipate kuja nyakati za ufufuko toka uso wa Bwana(Matendo 3:19)

**284.Na nani mwenye dhambi za kutubu?**

Mwenye dhambi za kutubu ni yule anayesikitika na kutubu dhambi zake na anayeamini mwokozi Yesu Kristo. Ndivyo ungano kunakuwa kuuzunika dhambi na imani kwa Injili.

697.Halafu utafurahi kwa zahibu za haki, kwa sadaka ya kuteketezwa, na sadaka nzima ya kutteketezwa; halafu watatoa ngombe ndume juu ya mazabahu yako.(Zaburi 51:19)

698.Wakamwambia: Amini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokolewa pamoja na nyumba yako.(Matendo 16:31)

## HISTORIA TAKATIFU

Zaburi 6, 32, 51 na 130: Ni mazaburi ya utubio wa Palestina wanatubu dhambi zao na wanaomba msamaha kwa Mungu.

Luka 15: 11 – 24: Mtoto moja akaomba msamaha kwa baba yake ya kwamba alifanya mabaya. Anafananishwa na mtu anaye uzunika juu ya dhambi yake na kuomba msamaha kwa Mungu.

Matayo 26: 31 –35, 69 –75: Petro anakuwa na uzuni kwa ajili ya dhambi yake na anauzunika sana.

**285.Ni matukio lazima gani ya kutubu kweli?**
Matukio ya lazima ya kutubu kwali, ni maisha ya kikristo ya kweli. Mtu aliye pokeya msamaha wa Mungu anaitwa kwa kubadirika namna ya kuishi kwake na kutenda kufatana na Neno la Mungu.

699.Basi zaeni matunda yanayofaa na toba(Matayo 3: 8)

## HISTORIA TAKATIFU

Wagalatia 5: 22 –26: Paulo anaonesha matunda zingine za kutubu za kweli.

Yakobo 2: 14 – 17: Matendo yetu inaonesha namna ya imani yetu.

**286.Nani anweza kukataliwa musamaha wa dhambi?**
Wanaweza kukataliya musamaha wa dhambi asioadhiwa, wakati anapokataa kutubu.

**2. MATUMIZI YA HUDUMA WA FUNGUO**

Unaamini nini kuhusu huduma wa funguo kufatana na Neno la kawaida?

Na amini ya kwamba wa tumishi wa Kristo, wanaitwa kwa huduma Mutakatifu kufanya kazi kati yetu panafasi ya Yesu kupitiya kwa ruhusa ya Mungu. Waki ifanya kufuatana na Neno la Mungu, hiyo itakuwa na bei, hata mbinguni, ni kama Bwana wetu Yesu Kristo alivyo ifanya mwenyewe. Hakika kwa upekee wanapotenga katika jamii ya kikristo waovu na wenye kukataa kuungama. Ni hakika pia wanapo samehe dhambi kwa wanao tubu na wenye kuhaidi mabadiriko ya mwenendo wao.

